
Haliuzwi
JANUARI 19, 2026
/islamicftz
Rajab 30 1447


# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 567

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Dkt. Mwinyi: Tendeni mema mtajwe vizuri mtakapokufa





## SHEIKH BANE:
# Uwezo kwenda Hijja haimaanishi utajiri

## Maimamu wakumbushana kuiandaa jamii kwa Ramadhan

## Rais Samia ahahidi kuliponya Taifa



"Serikali yangu imejipanga kutumia kipindi hiki cha pili kukarabati, kujenga upya na kulihuisha Taifa letu. Kwa Watanzania wenzangu, ghasia tulizozishuhudia sivyo tulivyo, sivyo kabisa. Kwa wadau wetu wa kimataifa, tunatambua ustahimilivu wa kidiplomasia. Tunaamini kwamba njia yetu itajengwa kwa msingi wa haki, majadiliano na heshima mpya katika mchakato wa kidemokrasia."

Rais Samia Suluhu Hassan

فتاوى
SHEIKH
Shaaban Mussa

Mageuzi ya Rais Samia itaimarisha imani ya jamii ya kimataifa

## Benki ya Dunia yatabiri ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.2 kwa Tanzania mwaka 2026

## Museveni aweka rekodi mpya urais Uganda



Ashinda Urais wa Uganda kwa muhula wa saba mfululizo

## Upotoshaji wa makusudi dhidi ya Sheikh Muhammad bin 'Abdul-Wahhab

## Saudi Arabia yatajwa uamuzi wa Marekani kutoshambulia Iran



## Donald Trump azidi kuwavuruga wenzie NATO




MWANDISHI WETU

# Sheikh Bane: Uwezo kwenda Hijja haimaanishi utajiri

KATIKA jitihada za kusahihisha dhana potofu ilioenea miongoni mwa Waislamu wengi, mwanazuoni Sheikh Twaha Suleiman Bane amebainisha kuwa ibada ya Hijja ni wajibu kwa kila mwenye uwezo wa safari, na kwamba uwezo huo haumaanishi lazima mtu awe na sifa ya "utajiri".

Sheikh Bane alitoa ufafanuzi huo hivi karibuni katika muhadhara maalum uliofanyika Masjid Hizbullah, Chiungutwa mkoani Mtwara, akisisitiza kuwa wito wa kwenda Hijja ni amri kutoka kwa Allah Aliyetukuka ambayo inahusu Waislamu wote wenye sifa za msingi.

## Maana ya uwezo

Akifafanua sintofahamu inayowafanya wengi kukwepa ibada hiyo, Sheikh Bane alisema tatizo kubwa ni uelewa usio sahihi wa neno la Qur'an "Manis-tata'a ilayhi sabila" (kwa anayeweza njia).

"Sisi tumehamishia 'sabiila' (njia) kwa maana ya utajiri, lakini Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ambaye ndiye mfasiri wa kwanza wa Qur'an, anasema ni kumudu masurufu; yaani matumizi yako njiani kwenda na kurudi, na kuwaachia familia yako mahitaji yao vizuri. Anayemiliki vitu hivyo, huyo tayari ameingia kwenye ulazima wa Hijja," alisema Sheikh Bane.

Aliongeza kuwa katika aya zote za Hijja, Allah hajatumia neno "matajiri", bali amewaita "watu". Hii ni tofauti na ibada ya Zaka ambapo Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliagiza ichukuliwe kutoka kwa matajiri na kupewa masikini.

## Hijja ni nguzo, si hiari

Sheikh Bane alikumbusha kuwa Hijja ni moja ya nguzo tano za Kiislamu na si jambo la hiari. Alinukuu kauli ya Allah katika Suratul Al-Imran: "Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea..." [Qur'an, 3:97].

Akielezea maana ya Hijja, Sheikh Bane alisema ni kukusudia safari kutoka mahali mtu alipo mpaka kufika Makka Tukufu kutekeleze matendo maalum katika maeneo maalum, kwa mtindo maalim na kwa wakati maalum kwa ajili ya kutafuta thawabu na kuitikia wito wa Allah.

"Sasa hili jambo unaloliona kama utalii fulani, kama mazoezo fulani ... litazame utakavyolitazama lakini Allah amelifaradhisha hili jambo lifanywe," Sheikh alisema na kuongeza kuwa hata Mtume naye alisema: "Enyi watu hakika Allah amefaradhisha Hijja juu yenu, basi mwende mkahiji."

"Aya inathibitisha ufaradhi, na hadith inathibitisha ufaradhi, lakini Hijja sio tu ni faradhi bali pia ni nguzo katika nguzo za Uislamu," alisema na kunukuu hadith maarufu ya Ibn Umar: Umejengwa Uislamu juu ya nguzo tano, ikiwemo Hijja.

Akifafanua zaidi uwajibu wa hijja, alisema huo Uislamu uliojengwa juu ya nguzo tano, maana yake kwa lugha rahisi ni kuwa mnyenyekevu na kufuata kikamilifu yale aliyokuja nayo Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), na katika hayo aliyokuja nayo Mtume ni hijja, ikiwa ni moja ya nguzo za Uislamu.

Alionya tabia ya baadhi ya Waislamu kuchagua ibada wanazozitaka na kuacha nyingine, akisema kuwa kufanya hivyo ni kufuata nyayo za Mayahudi na Manasara ambao walilaumiwa na Allah kwa kuamini baadhi ya kitabu na kukataa vingine.

Bane alinukuu aya ya Qur'an: [33: 36]: "Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi."

"Muislamu mwenye uwezo ni marufuku kwake kusema 'mimi nitafunga tu lakini siendi Hijja'. Huo si Uislamu. Uislamu ni unyenyekevu na kufuata kikamilifu yale aliyokuja nayo Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani)," alisisitiza.

Sheikh Bane aliwataka Muislamu ambao wanajijua kuwa Allah amewaruzuku wawe na mipango kwa ajili ya kutekelekeza Hijja, kama ambavyo wanakuwa na mipango mingine ya kusomesha watoto, kujenga makazi ya kujisitiri na kadhalika.

Akisisitiza umuhimu wa mipango, Sheikh Bane alisema Muislamu haifai kujitoa kabisa kuona hijja si yake kwa sababu aghlab "yale tunayoyaweza si kwa utajiri, ila yapo katika akili zetu, yamekaa katika nyoyo zetu, tunayafikirtia asubuhi na jioni, ndio maana ukipata nguvu unazielekeza huko."

## Manufaa na wito wa haraka

Sheikh Bane alihimiza kuharakisha kutekeleza hijja, akitaja kuwa hayo ni maelekezo ya Mtume, aliposema "Harakisheni kwenda Hijja (kwani) hakika mmoja wenu hajui kinaweza kumtokea nini huko mbele.

"Ima inaweza kudorora afya, ima ule uwezo unaweza kuharibika au Imani ikachafuka , Allah atuhifadhi, ukashindwa na hali ulishapata uwezo. Ukiondoka kiamani katika hali hiyo, unaondoka na deni.

"Na itokee hisani ya hao watoto wana dini wajue kuwa mirathi haigaiwi mpaka kwanza kutolewa alicho usia au kulipa deni vinginevyo watu watagawanagawana, watafanya yao, na wewe utakwenda kula mchanga ukiwa na deni la hijja hujalitekeleza."

Sheikh Bane alitaja manufaa anuai ya Hijja kuwa yanajumuisha ya kidunia (kibiashara na kijamii) na ya Akhera.

"Licha ya manufaa mengi ya kidunia, lakini kwa maelekezo ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani), 'Hijja inayotekelezwa kwa namna iliyo nzuri na sahihi haina malipo mengine ila Pepo' na 'Atakayehiji katika Nyumba hii, hakutenda machafu, wala hakutenda uovu wowote anarejea kama siku aliyozaliwa na mama yake (hana dhambi).'"

## Changamoto ya idadi ya mahujaji

Katika hatua nyingine, Sheikh Bane aligusia suala la kupunguzwa kwa mgao (quota) wa mahujaji kwa Tanzania kutoka 25,000 hadi kufikia takribani 20,000. Alibainisha kuwa jambo la kusikitisha ni kwamba tangu uhuru, Tanzania haijawahi kufikisha hata mahujaji 5,000 kwa mwaka mmoja.

رَجَب

HABARI
DAR ES SALAAM

MWANDISHI WETU

# Samia atoa ahadi za kuliponya Taifa

Rais Samia Suluhu Hassan amesema atatumia muhula wake wa pili madarakani kukarabati, kujenga upya na kulihuisha Taifa kufuatia vurugu zilizojitokeza wakati ya baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 29, 2025.

Rais Samia alisema hayo jana Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma wakati wa hafla ya kufungua mwaka pamoja na mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa Tanzania.

Katika hotuba yake, Rais Samia alizungumzia nyakati ngumu ambazo Tanzania imezipitia tangu uchaguzi ulipofanyika huku akitoa wito kwa mabalozi hao kushirikiana na Serikali sambamba na kuheshimu uhuru wa nchi.

Siku ya uchaguzi mkuu, kulizuka maandamano yaliyotawaliwa na vurugu, baadhi ya vijana waliolenga kuzuia uchaguzi huo, walikuwa wakichoma mali za umma na binafsi pamoja na kuharibu miundombinu hususani vituo vya mabasi yaendayo haraka (BRT).

Katika kukabiliana na watu hao, vyombo vya dola vilitumia nguvu kuwadhibiti waandamanaji hao kwa kuwapiga risasi.

Baadhi yao walipoteza maisha katika maandamano hayo huku wengine wakijeruhiwa.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Rais Samia amewaeleza mabalozi ili kuliponya Taifa, alisema amechukua hatua kadhaa, ikiwamo kuunda Wizara ya Vijana chini ya Ofisi ya Rais ili kujengea taasisi nguvu ya kizazi kijacho.

Pia, alisema ametoa msamaha kwa vijana 1,787 waliokamatwa kwa kuhusika na vurugu za siku ya uchaguzi.

Hatua nyingine alizozichukua, alisema ni kuunda Tume ya Kuchunguza Matukio Wakati na Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 na ahadi ya kuunda Tume ya Maridhiano ikiwa ni hatua ya kwenda kwenye mchakato wa kutengeneza Katiba mpya.

"Serikali yangu imejipanga kutumia kipindi hiki cha pili kukarabati, kujenga upya na kulihuisha Taifa letu.

"Kwa Watanzania wenzangu, ghasia tulizozishuhudia sivyo tulivyo, sivyo kabisa. Kwa wadau wetu wa kimataifa, tunatambua ustahimilivu wa kidiplomasia. Tunaamini kwamba njia yetu itajengwa kwa msingi wa haki, majadiliano na heshima mpya katika mchakato wa kidemokrasia," alisema.

> **"Kwa wale waliooonesha mshikamano na kutuma meseji za pongezi, tunawashukuru sana. Kwa wale ambao hawakufanya hivyo, tumechukua mrejesho wenu pia."**
>
> **Rais Samia Suluhu Hassan**

Rais Samia alisema Tanzania ni moja ya nchi ambazo uchumi wake unakuwa kwa kasi, ikiwa na ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) la asilimia sita huku mfumuko wa bei ukiendelea kuwa asilimia 3.3.

Kadhalika, alisema deni la Taifa limeendelea kuwa himilivu, uwiano wa deni katika GDP ukiwa ni asilimia 40.2, chini ya ukomo wa asilimia 55 kwa nchi za uchumi wa chini.

Katika hatua nyingine, Rais Samia aliwashukuru washirika wa kimataifa waliooonesha mshikamano na Tanzania wakati wa uchaguzi, hata hivyo amewataka wasioshiriki katika mtazamo wa Serikali kuheshimu uhuru wa nchi.

"Kwa wale waliooonesha mshikamano na kutuma meseji za pongezi, tunawashukuru sana. Kwa wale ambao hawakufanya hivyo, tumechukua mrejesho wenu pia.

"Ninawaomba marafiki wetu kutoa ushirikiano katika mabadiliko yetu na kwa wale ambao hawatashiriki mtazamo wetu, ninaomba angalau uhuru wetu kama nchi," alisema mkuu huyo wa nchi katika hotuba yake.



Baadhi ya mabalozi na viongozi mbalimbali wakiwa katika Sherehe ya Mwaka Mpya kwa Mabalozi iliyofanyika Ikulu ya Chamwino, Dodoma jana. Picha na Ikulu




HABARI
DAR ES SALAAM

MWANDISHI WETU

# Benki ya Dunia yatabiri ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.2 kwa Tanzania mwaka 2026

**Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kukua kwa takriban asilimia 6.2 mwaka huu, na kuiweka nchi hiyo miongoni mwa nchi tatu zinazoongoza kwa ukuaji wa uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kwa mujibu wa ripoti ya hivi karibuni ya Global Economic Prospects ya Benki ya Dunia.**

Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kukua kwa takriban asilimia 6.2 mwaka 2026, hali itakayoiweka nchi hiyo miongoni mwa nchi tatu zinazoongoza kwa ukuaji wa uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kwa mujibu wa Benki ya Dunia.

Katika ripoti yake ya hivi karibuni ya Global Economic Prospects 2026, Benki ya Dunia inatabiri kuwa Rwanda pekee ndiyo itakayokua kwa kasi zaidi ndani ya jumuiya hiyo, kwa takriban asilimia 7.2, ikichochewa na uwekezaji endelevu katika sekta za huduma, ujenzi na teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT).

Uganda inatarajiwa kukua kwa takriban asilimia 6.4 huku shughuli katika sekta ya mafuta zikizidi kushika kasi.

Kenya, ambayo kwa jadi imekuwa nguzo ya ukuaji wa uchumi wa kanda, inatarajiwa kubaki nyuma kwa ukuaji wa asilimia 4.9, ikikabiliwa na ukandamizaji wa matumizi ya kifedha ya serikali na mzigo mkubwa wa kuhudumia deni.

Burundi pia inatabiriwa kukua kwa asilimia 4.9, ishara ya kupona taratibu kwa uchumi wake, ingawa bado ni chini ya kasi inayohitajika kupunguza pengo la kipato kati yake na majirani zake.

Mtazamo wa Benki ya Dunia kwa ujumla unaendana na tathmini za Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ambazo zinaonesha kuendelea kwa kasi ya uchumi wa ndani.

Kwa mujibu wa benki kuu, ukuaji wa uchumi ulifikia asilimia 5.9 mwaka 2025, ukichangiwa na sekta za kilimo, madini na ujenzi. Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.8, ukichochewa na ujenzi, utalii na viwanda.

Kwa robo ya kwanza ya mwaka 2026, BoT inatabiri uchumi wa Tanzania Bara kukua kwa asilimia 6, huku uchumi wa Zanzibar ukitarajiwa kukua kwa asilimia 7.2.






MWANDISHI WETU

# Dkt. Mwinyi: Tendeni mema mtajwe vizuri mtakapokufa



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Hussein Ali Mwinyi amewanasihi Waumini wa Dini ya Kiislamu Kutenda Mambo Mema ili kutajwa kwa Wema ndani ya Jamii pale wanapotangulia mbele ya Haki.

Alhaji Dkt, Mwinyi ameyasema hayo leo tarehe 16 Januari 2026 alipojumuika na Waumini wa Dini ya Kiislamu katika Ibada ya Sala ya Ijumaa iliyosaliwa Msikiti wa Bamita Chumbuni ,Mkoa wa Mjini Magharibi

Kwa Mnasaba huo ,Alhaji Dkt, Mwiyi amesema Serikali imekuwa Ikiendeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo nchini kote ikiwa ni juhudi za Serikali kuhakikisha inatimiza Matarajio Makubwa walionayo Wananchi. Naye Katibu Mtendaji wa Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar , Sheikh Khalid Ali Mfaume ametoa Wito kwa Waumini wa dini ya Kiislamu kutafuta Elimu zaidi ili kujijengea Heshima ndani ya Jamii.

Naye, Khatibu wa Msikiti huo Sheikh Suleiman Nassor amewasihi Waumini wa Dini ya Kiislamu kuzidisha Upendo na Umoja baina yao pamoja na kutafuta Elimu kwani ni muhimu kwa Maisha ya kila siku ya Mwanadamu pamoja na Kuwahimiza kuzidisha Ibada katika Miezi Mitukufu katika Dini ya Kiislamu. Aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Ali Hassan Mwinyi aliweka Jiwe la Msingi na Kusali katika Msikiti huo wa BAMITA Mwaka 1981.

Alhaji Dkt, Mwinyi amnaendeleza Utaratibu wake wa kujumuika na Waumini wa Dini ya Kiislamu katika Sala ya Ijumaa katika Misikiti mbalimbali Mjini na Vijijini.




MWANDISHI WETU

# Maimamu wakumbushana kuiandaa jamii kwa Ramadhan

Umoja wa Maimamu na Walimu wa Madrasa Tanzania UMATA umekumbusha wanachama wake kuanza maandalizi ya Ramadhan kwa kuiasa jamii kujiandaa mapema kwa mahitaji muhimu na kwa uchamungu.

Wito huo umetolewa kupitia kundi la WhatsApp la umoja huo na kusambazwa pia kwenye mitandao mingine ya kijamii, ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa maimamu kubadilishana maarifa juu ya masuala muhimu ya kuzingatia katika khutba za Ijumaa.

Katika tamko hilo lililopewa kichwa "Salamu za Ijumaa kutoka UMATA", maimamu na walimu wa madrasa waliombwa kutumia khutba za Ijumaa ya leo kuangazia masuala ya msingi yanayoigusa jamii ya Kiislamu, hasa kipindi hiki cha kuanza kwa muhula wa shule na maandalizi ya mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Tamko hilo limeelekeza umuhimu wa kuangalia mahudhurio ya wanafunzi katika Swala ya Ijumaa baada ya kufunguliwa kwa shule, na kulinganisha hali hiyo na kipindi cha likizo

Kadhalika, UMATA imewakumbusha wazazi kuwajibika kuhakikisha watoto wao wanaswali Ijumaa, ikisisitiza kuwa jambo hilo ni muhimu katika malezi ya dini.

Pia maimamu wameombwa kuhamasisha waumini kuwasaidia watoto yatima na wanaotoka katika familia duni waliokwama kuendelea na masomo. Misikiti imetakiwa kutoa taarifa ya idadi ya watoto waliokwisha saidiwa na wanaohitaji msaada zaidi.

Kuhusu Ramadhan, UMATA imesisitiza kuwa maandalizi ya futari na daku kwa wahitaji yaanze sasa kwa kupanga bajeti na kutafuta mahitaji. Aidha, wazazi wamekumbushwa kuchangia chakula cha Ramadhan kwa watoto wao shuleni na kuepuka kulea tabia ya kusubiri misaada hata kwa yale yaliyo ndani ya uwezo wao.

## Samia aeleza maendeleo ya SGR, bomba la mafuta

**Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kazi inayoendelea kwa sasa ni ukamilishaji wa Reli ya Kisasa (SGR) na Mfereji wa Mafuta wa Ghuba ya Afrika Mashariki, ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2026.**

**Amesema Serikali itahakikisha inazingatia na kuongeza thamani, uwezo wa kuuza nje, na uundaji wa ajira kupitia maeneo maalumu ya kiuchumi, ukihusisha miundombinu na mifumo ya viwanda.**

**Rais Samia aliyasema hayo Januari 15 alipokuwa akizungumza na makamishna wakuu, mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa katika Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma. "Ujumbe wetu ni wazi, Tanzania inahamia kutoka kuuza malighafi kwenda kuuza thamani halisi. Katika mkakati huu, bandari na milango ya biashara zina nafasi muhimu sana," alisema Rais Samia.**

## TIPSO yanoa walimu

**Jumuiya ya Shule za Msingi za Kiislamu TIPSO imeendesha semina ya siku mbili ya kuwajengea uwezo walimu wa masomo yote, ikiwa ni maandalizi ya utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa kwa lengo la kuinua ubora wa ufundishaji na matokeo ya wanafunzi.**

**Semina hiyo imeanza Jumamosi, Januari 17, 2026 katika kituo cha elimu Yemen Schools – DYCCC ambapo katika siku ya kwanza ilishuhudia mwitikio mkubwa wa walimu kutoka shule nyingi za msingi za Kiislamu za Dar es Salaam na Pwani.**

**Akifungua semina hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa TIPSO, Sheikh Salim Baabde, aliwataka walimu kutumia fursa hiyo kuboresha nyaraka za maandalizi ya kufundishia, mbinu za kufundisha na tathmini ili kuendana kikamilifu na mtaala ulioboreshwa.**

**Sheikh Baabde al;isisitiza kuwa maandalizi bora ndiyo msingi wa matokeo bora shuleni.**

**Semina hiyo pia inashirikisha wataalamu wa mitaala kutoka taasisi za elimu, wakitoa mafunzo ya vitendo kuhusu upangaji wa somo, malengo ya kujifunza, na mbinu shirikishi darasani.**

**Kwa mujibu wa waandaaji, mafunzo haya yanalenga kuziimarisha shule za msingi za Kiislamu na shule nyinginezo katika utekelezaji wa mtaala na kuongeza ushindani wa kitaaluma.**

## Mchengerwa atoa maagizo 17 kuelekea Bima ya Afya kwa wote

**Waziri wa Afya, Mohamed Mchengerwa ametoa maagizo 17 kwa watendaji wa wizara na taasisi zilizo chini yake, huku akisisitiza hatamvumilia mtumishi mzembe na badala yake atamlinda yeyote atakayetoa maamuzi ya haki.**

**Miongoni mwa maagizo hayo ni kuwepo kwa matumizi ya mifumo inayosomana katika taasisi zote, ubora wa huduma za matibabu, na kuwa na malengo ya lazima ili mpango wa bima ya afya kwa wote usiwe zimamoto bali endelevu. Pia amepiga marufuku matumizi makubwa ya Sh 20 bilioni kwa ajili ya mitihani akitaka yakomeshwe mara moja.**

**Waziri Mchengerwa ametoa maagizo hayo Januari 14, 2026 wakati akihutubia kwenye kikao kazi baina yake na watendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya na watumishi wa afya wa Mkoa wa Dodoma, kilichofanyika katika viwanja vya Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma.**

**Katika hotuba yake, Waziri Mchengerwa alisema utoaji wa huduma bora za afya ni msingi wa heshima ya maisha ya binadamu hivyo haupaswi kuathiriwa na uzembe, ucheleweshaji wa maamuzi au udhaifu wa mifumo ya uendeshaji wa hospitali.**

**Alisema wananchi wanaofika hospitalini wanapaswa kupata huduma bora bila visingizio, akibainisha kuwa imani ya mwananchi katika mfumo wa afya hujengwa na kuvunjwa kupitia namna huduma inavyotolewa.**

**Kuhusu bima ya afya kwa wote, Waziri Mchengerwa alisema uzinduzi wake utafanyika ndani ya kipindi cha siku 100 za Rais Samia, na hapo huduma itaanza kutolewa.**

**Alisema suala la bima ya afya kwa wote halipaswi kupimwa kwa muhula mmoja wa uongozi badala yake tathmini iwe ya muda mrefu kidogo na kutaka mwanzo wa yote uwe ni kuzalisha wataalamu wenye ujuzi na uwezo wa kuhudumia wagonjwa ili kuondoa manung'uniko.**






UKHTI FATIMA SS

# Mageuzi ya Samia itaimarisha imani ya jamii ya kimataifa

**■ Kauli na hatua za Rais zimeanza kubadili taswira ya Tanzania kutoka nchi iliyotazamwa kwa tahadhari hivi karibuni hadi mshirika anayejifunza kutokana na yaliyopita na kujielekeza kwenye mustakabali wake.**

Mageuzi ya kisiasa yaliyoahidiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, yanairejeshea nchi imani ya jamii ya kimataifa, hasa katika eneo la utawala, maridhiano ya kisiasa na heshima ya taasisi za kidemokrasia.

Kauli na hatua za Rais zimeanza kubadili taswira ya Tanzania kutoka nchi iliyotazamwa kwa tahadhari hivi karibuni hadi mshirika anayejifunza kutokana na yaliyopita na kujielekeza kwenye mustakabali wake.

Katika hotuba yake kwa mabalozi na wakuu wa mashirika ya kimataifa iliyotolewa Ikulu Chamwino, Dodoma, Rais Samia alisisitiza dhamira ya serikali yake katika maridhiano ya kitaifa, mageuzi na ujenzi upya wa taasisi, akirejea wazi matukio ya kisiasa yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi wa Oktoba 2025. Alieleza kuwa serikali imejipanga kuhakikisha haki, uwajibikaji na marekebisho ya kikatiba yanapewa nafasi kupitia mifumo shirikishi na ya maridhiano

Miongoni mwa hatua zilizobeba uzito wa kisiasa ni msamaha wa rais kwa wafungwa 1,787 waliokuwa wanahusishwa na machafuko ya baada ya uchaguzi, pamoja na kuundwa kwa Tume Huru ya Uchunguzi kwa lengo la kujifunza, kurekebisha na kuimarisha mifumo ya haki. Hatua hizi zimefasiriwa na wadau wa nje kama ishara ya utayari wa serikali kukubali dosari na kuchukua hatua za kurejesha imani ya wananchi na jumuiya ya kimataifa.

Aidha, ahadi ya kupitia upya mfumo wa kikatiba na kisiasa kwa misingi ya maridhiano imeonekana kama dira ya kuijenga Tanzania jumuishi, inayokubali tofauti za kisiasa bila migongano. Kauli ya Rais Samia kwamba "Tanzania ni taifa lililojifunza kutoka katika yaliyopita na linaangalia mbele" imekuwa ujumbe mzito kwa mabalozi na washirika wa maendeleo.

## Uchumi mambo safi – wakua kwa asilimia 5.9

Tanzania inaendelea kuwa miongoni mwa nchi za Afrika zenye ukuaji wa haraka wa uchumi, kwa ukuaji wa Pato la Taifa la ndani (GDP) kwa asilimia 5.9, huku mfumuko wa bei ukiwa imara kwa asilimia 3.3.

Aidha, deni la taifa linaendelea kudumishwa katika kiwango endelevu, ambapo uwiano wa deni dhidi ya Pato la Taifa (Debt-to-GDP ratio) umefikia asilimia 48.2, chini ya kiwango cha kizingiti cha asilimia 55 kwa nchi za kipato cha chini.

Takwimu hizo zimetolewa Januari 14, 2026 na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuwa akizungumza na makamishna wakuu, mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa katika Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma.



Rais Samia ameeleza kuwa Soko la Mitaji ya Taifa pia limeendelea kustawi ambapo Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) limeona ongezeko la 34.3% katika thamani ya soko, kufikia Sh trilioni 23,995.45 mwishoni mwa mwaka uliopita.

Pia, Tanzania imeendelea kupata alama za mkopo zenye mvuto, ikiwa ni B1 kutoka Moody's, na B+ kutoka Fitch, jambo linaloashiria kujiamini kwa wawekezaji, gharama za mkopo kuwa chini, na uimara wa uchumi.

"Hii ni hatua chanya katika kujenga kujiamini kimataifa na kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI). Tunaendelea kuhakikisha marekebisho ya utawala bora, kupunguza uhaba wa fedha za kigeni, na kuboresha uwiano wa kodi dhidi ya Pato la Taifa," ameeleza Rais Samia.

Kwa mtazamo huo chanya, miradi mipya 927 ya uwekezaji iliwekwa kwenye rejista mwezi Desemba 2025 ikiwa na thamani ya jumla ya zaidi ya Dola za Marekani bilioni 11.09, ikionyesha ongezeko la asilimia 19.03 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.

Rais Samia ameeleza kuwa idadi hii ya miradi mipya 927 ni rekodi ya juu zaidi ya miradi iliyosajiliwa katika mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwa Wakala wa Kukuza Uwekezaji Tanzania, ikivunja rekodi ya miradi 901 ya mwaka 2024.

Shiriki la wawekezaji wa ndani pia limeendelea kuwa imara, kwani miradi 288 sawa na asilimia 31.07 inatarajiwa kutekelezwa na wawekezaji wa ndani, ikionyesha kuongezeka kwa kujiamini kwa wajasiriamali wa Tanzania.

"Aidha, mwaka 2025 tumeendelea na safari yetu ya viwanda tukishuhudia ukuaji wa sekta muhimu za uchumi. Sekta zinazoongoza ni pamoja na kilimo ambapo tumeendelea kuona ongezeko la uzalishaji na uwiano wa uhakika wa chakula (food self-sufficiency ratio) kufikia asilimia 128 katika mwaka wa fedha 2024/2025 ikiwa ni ongezeko la takriban 3.2%," alisema Rais Samia.

Aliongeza kuwa shughuli za madini zimeongezeka kwa asilimia 48.27 kutoka Sh trilioni 10.6 mwaka 2023/2024 hadi Sh trilioni 15.8 mwaka 2024/2025, zikichangiwa hasa na dhahabu, makaa ya mawe na madini ya ujenzi na viwandani.




# Sababu zatajwa ukuaji soko la Takaful duniani

■ **"Soko la Takaful linatarajiwa kukua hadi Dola bilioni 72.5 mwaka 2035, wastani wa ongezeko la 6.9% kwa mwaka."**




Soko la Takaful duniani linaendelea kukua kwa kasi, likionyesha mwelekeo chanya katika sekta ya bima ya Kiislamu.

Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa katika tovuti ya Industry Today ya Uingereza Januari 17, 2026, soko la Takaful linatarajiwa kukua kutoka thamani ya Dola bilioni 34.9 mwaka 2024 hadi Dola bilioni 72.5 ifikapo mwaka 2035, likionyesha ongezeko la wastani la asilimia 6.9 kwa mwaka.

Hii, kwa kiasi kikubwa, inatokana ongezeko la mahitaji ya bima zinazokubaliana na misingi ya Shariah na ongezeko la uelewa wa bidhaa za kifedha zenye maadili.

Ukuaji wa soko la Takaful unasukumwa na sababu kadhaa kuu zinazofuatana. Kwanza, kuna ongezeko la uelewa na kukubalika kwa bidhaa za kifedha zinazozingatia Shariah, hasa miongoni mwa jamii za Waislamu na wale wanaopendelea mifumo ya kifedha yenye maadili, uwazi na haki.

Pili, mahitaji ya bima ya afya, maisha na mali yameongezeka, hususan katika nchi zinazoendelea ambako athari za magonjwa, majanga ya asili na changamoto za kiuchumi zimeongeza uhitaji wa ulinzi wa kifedha.

Sababu nyingine muhimu ya ukuaji ni msaada wa moja kwa moja wa serikali na mifumo rafiki ya kisheria katika baadhi ya nchi. Nchi kama Malaysia imeweka mfumo thabiti wa kisheria unaounga mkono Takaful kupitia Benki Kuu (Bank Negara Malaysia), na kuifanya kuwa soko lililokomaa.

Katika nchi za Ghuba (GCC) kama Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Qatar na Bahrain, serikali zimehimiza matumizi ya Takaful kupitia sera za bima za lazima, ushiriki wa taasisi za umma na marekebisho ya sheria za bima.

Vilevile, Indonesia na Pakistan zimechukua hatua za kisera kuimarisha sekta ya bima ya Kiislamu kama sehemu ya mfumo mpana wa fedha za Kiislamu.

Kwa upande wa mgawanyo wa soko, Takaful imegawanyika katika Takaful ya jumla na Takaful ya familia. Takaful ya jumla inahusisha ulinzi wa mali, magari na afya, huku Takaful ya familia ikilenga akiba, uwekezaji na ulinzi wa maisha. Huduma hizi husambazwa kupitia benki, mawakala wa bima, madalali pamoja na majukwaa ya kidijitali, ambayo yanazidi kupata umaarufu kutokana na urahisi na upatikanaji wake.

Hata hivyo, pamoja na ukuaji huo, soko la Takaful linakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwemo uelewa mdogo wa jamii katika baadhi ya nchi, tofauti za mifumo ya kisheria baina ya mataifa, pamoja na ushindani kutoka kwa bima za kawaida. Pia, uhaba wa wataalamu waliobobea katika bima za Kiislamu unaendelea kuwa kikwazo katika upanuzi wa haraka wa sekta hii.

Kwa mtazamo wa baadaye, soko la Takaful linaonesha matumaini makubwa, hasa katika Asia ya Kusini Mashariki, Mashariki ya Kati na Afrika. Mageuzi ya kidijitali, bidhaa bunifu kama micro-Takaful, pamoja na ushirikiano kati ya kampuni za bima, benki na taasisi za kifedha, vinatarajiwa kuimarisha zaidi upatikanaji wa huduma.

Kwa ujumla, Takaful inaendelea kujijenga kama mbadala imara wa bima za kawaida, unaochanganya ulinzi wa kifedha na misingi ya maadili ya Kiislamu.






NA MWANDISHI WETU

# Waganda wamrejesha madarakani Museveni

**Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2006 ulikuwa wa kwanza wa vyama vingi baada ya miaka 25 nchini Uganda. Museveni alishinda kwa kupata asilimia 59 ya kura za urais na chama chake, NRM, kilipata wingi wa viti vya ubunge. Mwanamuziki maarufu na kiongozi wa upinzani Bobi Wine alimkabili Museveni katika uchaguzi wa urais wa mwaka 2021 na Museveni na aliibuka mshindi na sasa anaelekea...**


Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni, ameshinda tena kiti cha urais na kurejea madarakani kwa muhula wa saba, matokeo rasmi yakionyesha amepata asilimia 71.65 ya kura katika uchaguzi wa rais uliofanyika Alhamisi, Januari 15, 2026.

Ushindi huo unamruhusu kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 81 kuendelea kuongoza taifa hilo kwa kipindi kirefu zaidi, baada ya kuingia madarakani mwaka 1986.

Kwa mujibu wa matokeo ya Tume ya Uchaguzi, mpinzani wake mkuu, Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobi Wine (miaka 43), alipata takribani asilimia 24.72.

Mara baada ya kutangazwa kwa matokeo, Wine alitangaza kuyakataa, akidai kulikuwa na dosari na vitisho dhidi ya upinzani pamoja na madai ya kujazwa kwa kura.

Aidha, alieleza kuwa alikuwa akijisitiri baada ya kile alichodai kuwa ni uvamizi wa majeshi ya usalama nyumbani kwake, huku polisi wakikanusha madai hayo na kusema ulinzi uliwekwa eneo hilo kwa sababu za kiusalama.



Uchaguzi huo uligubikwa na sintofahamu baada ya ripoti za vifo, vitisho na kukamatwa kwa baadhi ya watu wanaodaiwa kuwa wa upinzani, pamoja na kuzimwa kwa huduma ya intaneti kuanzia Jumanne kabla ya siku ya kupiga kura.

Waangalizi wa uchaguzi kutoka Afrika walisema walipokea taarifa za vitisho, kukamatwa na utekaji nyara vilivyochangia "kuingiza hofu" na kupunguza imani ya umma katika mchakato wa uchaguzi, ingawa walisema siku ya kupiga kura kwa ujumla ilikuwa tulivu maeneo mengi.

Katika taarifa yake ya Januari 17, 2026, Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AUC), Mheshimiwa Mahmoud Ali Youssouf, aliipongeza Uganda kwa kuendesha uchaguzi na akampongeza Museveni kwa kuchaguliwa tena, akitaja pia mchango wa ujumbe wa uangalizi ulioongozwa na aliyekuwa Rais wa Nigeria, Goodluck Jonathan, chini ya ushirikiano wa AU, COMESA na IGAD.

Wachambuzi wengi wamekuwa wakitazama uchaguzi huo kama wenye mwelekeo unaojulikana kutokana na nguvu kubwa ya chama tawala na udhibiti wa vyombo vya dola, huku upinzani ukiendelea kudai mazingira hayakuwa sawa.

Hali ya ulinzi iliimarishwa katika mji mkuu Kampala kuzuia maandamano, wakati wito ukiendelea kutolewa kwa pande zote kuheshimu amani na sheria.

NA MWANDISHI WETU

# Saudi Arabia yatajwa uamuzi wa Marekani kutoshambulia Iran



**Uamuzi wa Rais wa Marekani Donald Trump wa kusitisha mipango ya mashambulizi ya kijeshi dhidi ya Iran umeanza kuchukuliwa kama ushindi wa diplomasia ya nchi za Kiarabu, hususan Saudi Arabia, Qatar, Misri na Oman.**

Ripoti za kimataifa zinaeleza kuwa mataifa hayo yalifanya ushawishi wa pamoja kwa Washington, yakionya kuwa shambulio lolote dhidi ya Iran lingeweza kusababisha mgogoro mkubwa wa kikanda wenye athari za kiusalama na kiuchumi duniani.

Saudi Arabia, kupitia Waziri wake wa Nchi Adel al-Jubeir, ilisisitiza msimamo wake wa muda mrefu kwamba migogoro ya kikanda inapaswa kutatuliwa kwa mazungumzo, si kwa nguvu za kijeshi.

Kauli hiyo imekuja katika kipindi ambacho Mashariki ya Kati bado ina kumbukumbu chungu za vita vya uwakala na mashambulizi ya makombora na ndege zisizo na rubani yaliyohusishwa na makundi yanayoungwa mkono na Iran.

Katika wiki za karibuni, Trump alitoa kauli kali akionya kuwa Marekani iko tayari kuingilia kati iwapo Iran ingewakandamiza waandamanaji waliokuwa wakipinga hali ngumu ya uchumi.

Iran, kwa upande wake, kupitia viongozi wa juu wa usalama, ilitishia kujibu kwa nguvu endapo ingerushiwa mashambulizi, ikiwemo kulenga maslahi ya Marekani na washirika wake katika eneo hilo.

Hata hivyo, hali ilibadilika ghafla baada ya ripoti kuibuka kuwa Iran ilisimamisha utekelezaji wa hukumu za kifo dhidi ya wafungwa wa kisiasa waliokuwa wanahusishwa na machafuko ya hivi karibuni.

Trump mwenyewe alipunguza uzito wa ushawishi wa Waarabu akisema kuwa alijishawishi binafsi, akitaja kusitishwa kwa hukumu hizo kama sababu kuu ya kupunguza makali ya msimamo wake.

Licha ya kauli hiyo, wachambuzi wa siasa za kimataifa wanaona kuwa msimamo wa Saudi Arabia na washirika wake ulikuwa na mchango mkubwa.

Hofu kubwa ilikuwa ni kwamba vita kamili dhidi ya Iran vingehatarisha miundombinu muhimu ya mafuta na nishati katika Ghuba, jambo ambalo lingeutikisa uchumi wa dunia kwa kasi isiyotarajiwa.

Ikumbukwe kuwa Saudi Arabia na Iran zimekuwa mahasimu wa muda mrefu, zikitofautiana kuhusu masuala ya Syria, Yemen na Lebanon. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni Riyadh imechukua mkondo wa kupunguza mvutano, ikihamia kwenye diplomasia na mazungumzo badala ya makabiliano ya moja kwa moja.

Kauli ya balozi wa Saudi Arabia katika Umoja wa Mataifa imeweka wazi mantiki hiyo: licha ya historia ya mashambulizi na vitisho, Saudi Arabia imechagua utulivu kwa kutambua kuwa vita katika eneo hili mara nyingi huwaletea madhara makubwa raia wa kawaida kuliko wanasiasa.

Kwa mtazamo wa kiuchambuzi, kusitishwa kwa mashambulizi dhidi ya Iran ni ushindi wa muda wa diplomasia ya Kiarabu. Hata hivyo, mvutano bado upo, na mustakabali wa amani ya kudumu utategemea zaidi kama pande zote zitadumisha mazungumzo na kujiepusha na siasa za vitisho.

NA MWANDISHI WETU

# Trump awavuruga wenzie Mataifa ya Magharibi



Maandamano makubwa ya Januari 17, 2026 huko Greenland na Denmark yameweka wazi ukubwa wa mpasuko unaojitokeza ndani ya kambi ya Magharibi baada ya Rais wa Marekani Donald Trump kusukuma wazo la Marekani "kuchukua" Greenland—eneo lenye utawala wa ndani chini ya Ufalme wa Denmark.

Waandamanaji Nuuk na Copenhagen walibeba mabango yenye ujumbe mfupi lakini mzito: "Greenland is not for sale" (Greenland siyo ya kuuzwa).

Kinachofanya mgogoro huu kuwa nyeti zaidi ni mchanganyiko wa siasa za usalama na shinikizo la kiuchumi. Reuters imeripoti kuwa Trump hajafuta uwezekano wa matumizi ya nguvu katika kauli zake za kuhusisha Greenland na "usalama wa taifa" la Marekani.

Kisha akapandisha joto kwa kutangaza ushuru (tariffs) kwa washirika wa Ulaya wanaopinga mpango wake: kuanzia Februari 1 bidhaa kutoka Denmark, Norway, Sweden, Ufaransa, Ujerumani, Uholanzi, Finland na Uingereza zitozwe 10%, na ushuru huo uongezwe hadi 25% kuanzia Juni 1 "mpaka makubaliano yafikiwe" ya "ununuzi kamili" wa Greenland.

Hatua hii imeonekana kama jaribio la kugeuza "mzozo wa eneo" kuwa vita ya biashara, jambo linaloweza kuyumbisha mshikamano wa NATO na uhusiano wa kuvukana Atlantiki.

Kwa Denmark, suala si rasilimali pekee, bali ni mamlaka na hadhi ya dola: Denmark bado inasimamia ulinzi na mambo ya nje ya Greenland, ingawa Greenland ina utawala wa ndani.

Ndani ya Greenland, vyama vyote vya bunge vimeripotiwa kuunga mkono wazo la uhuru wa baadaye, lakini wakisisitiza maamuzi yafanywe na WaGreenland wenyewe—si kwa shinikizo la kigeni.

Wakati huo huo, ujumbe wa wabunge wa Marekani uliokuwa Copenhagen uliongeza uzito wa tukio. Seneta Chris Coons, anayetajwa kuongoza ujumbe huo, alisema kauli za Trump "not constructive" (si za kujenga), akijaribu kutuliza hofu za washirika wa Denmark.

Hii inaashiria kuwa hata ndani ya taasisi za Marekani kuna wanaoona njia ya vitisho inaweza kuharibu uaminifu wa muda mrefu wa muungano.

Ushirika wa wachawi waanza kupasuka

Kwa upande wa pili wa Atlantiki, mfano mwingine unaoonyesha mtikisiko wa Magharibi ni hatua ya Canada kufungua mlango mpana zaidi wa biashara na China—ikiwa ni ishara kwamba washirika wa Marekani sasa wanatafuta "bima" dhidi ya kutotabirika kwa sera za Washington.

Waziri Mkuu Mark Carney ameeleza mwelekeo huu kwa kauli: "We take the world as it is, not as we wish it to be."

Katika makubaliano ya awali na China, Canada imekubali kuruhusu hadi magari ya umeme (EV) 49,000 kutoka China kuingia kwa ushuru wa 6.1%, ikishusha ushuru mkubwa uliowekwa 2024 (100%).

Kwa upande wake, China imekubali kupunguza ushuru wa kulipiza kisasi kwa bidhaa za Canada—ikiwemo canola na baadhi ya bidhaa za baharini—kwa muda maalum, hatua inayotafsiriwa kuwa unafuu kwa wakulima na wauzaji wa nje.

Lakini Canada imeingia katika mjadala mkali wa ndani: viongozi wa Ontario (kitovu cha sekta ya magari) wameonya kuwa EV za bei nafuu zinaweza kuathiri ajira, huku maeneo ya Prairie yakiona mkataba huu kama "habari njema" kwa wakulima.

Marekani pia imeonyesha wasiwasi, ikitaja uamuzi huo kuwa tatizo, ishara kwamba mgawanyiko wa kibiashara unaweza kugeuka mgogoro wa kimkakati.

Kuanzia Greenland hadi mkataba wa Canada–China, picha inayojitokeza ni moja: mbinu ya Trump ya kutumia vitisho na ushuru inawasukuma washirika wa Magharibi kujipanga upya—wengine wakipaza sauti mitaani, wengine wakitafuta masoko mapya.

Matokeo yake yanaweza kuwa Magharibi yenye sauti nyingi, yenye mashaka zaidi, na yenye mshikamano unaojaribiwa kwa njia ambayo haijazoeleka kwa miongo kadhaa.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania
Mhariri
+255 789 201383

# Tuutumie mwezi wa Shaaban kujiandaa na Ramadhan

Tunakaribia kuupokea mwezi wa Shaaban wenye hadhi kubwa na nafasi maalum katika Uislamu. Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) alikuwa akifanya ibada mbalimbali ndani ya mwezi huu, ikiwamo funga, dua na mema mengine kwa ujumla wake kwa ajili ya kufaidika na mwezi huu.

Katika mwezi huu, Muislamu anatakiwa ajihimu katika kufanya ibada ikiwa ni njia mojawapo ya kujiandaa zaidi na Ramadhan. Wanazuoni (Allah awarehemu) wamesema kuwa, mwezi huu umeitwa Shaaban kwa sababu Waarabu walitawanyika katika mwezi huu kutafuta maji au kupigana baada ya kupumzika katika mwezi Mtakatifu wa Rajab.

Fadhila za mwezi wa Shaaban

Mwezi wa Shaaban una fadhila kubwa kutokana na jinsi Mtume (rehema za Allah na amani iimshukie) alivyouenzi hadi kufikia kuitwa 'Shahrul Muswtwafaa' yaani mwezi wa Mtume. Imepokewa hadith kutoka kwa Usama bin Zayd (Allah amridhie yeye na baba yake) akisema, alimuuliza mjumbe wa Allah: "Ewe mjumbe wa Allah, sijapata kukuona ukifunga swaumu katika miezi mingine kama unavyofunga katika (mwezi wa) Shaaban!"

Mtume akasema: "Huo ni mwezi ambao watu wengi wanaghafilika. Nao upo baina ya Rajab na Ramadhan. Nao ni mwezi ambao matendo (ya viumbe) huinuliwa kwenda kwa Mola wa Ulimwengu. Basi napenda amali zangu ziinuliwe huku nikiwa nimefunga swaumu." [Abu Daudi na Nasa'iy].

Na imepokewa hadith nyingine kutoka



kwa Anas bin Malik (Allah amridhie) akisema: "Alikuwa mjumbe wa Allah akifunga pasina kuacha siku mpaka tunasema, 'Mtume hatofungua mwaka huu'. Kisha anafungua na hafungi tena mpaka tunasema, 'Mtume hatafunga mwaka huu.' Na mwezi aliopendelea zaidi kufunga ni Shaaban." [Ahmad].

Hadith hizi zinaonesha kuwa, Shaaban ndiyo mwezi ambao matendo ya waja yanainuliwa kwenda kwa Muumba wao. Mwezi huu ni kama mwezi wa kufunga hesabu ya matendo ya waja. Kwa mwaka huu, 1447 Hijriya, hesabu zetu zitafungwa siku ya mwisho ya Shaaban.

Tunapaswa kujiuliza, je ni kwa amali gani tutazifunga kurasa za hesabu zetu kwa mwaka huu? Kauli ya Mtume kwamba: "Huo (mwezi wa Shaaban) ulio baina ya Rajab na Ramadhan ni mwezi ambao watu wengi hughafilika," inatufundisha kwamba, kufanya ibada wakati watu wameghafilika na Allah kuna fadhila kubwa.

Ndiyo maana kusali usiku wakati watu wamelala kuna fadhila kubwa na thawabu nyingi. Lakini pia tunatoa tahadhari kwamba, tukiamua kufanya ibada kwa wingi katika mwezi wa Shaaban, basi tufanye hivyo kwa kutafuta radhi za Allah Aliyetukuka peke yake na si kuonesha uhodari wetu wa kufanya ibada.

Ni vema tukumbuke kwamba kama hatukuweka nia ya kufunga swaumu kuanzia mwanzo wa Shaaban, ikishafika nusu ya mwezi huo basi hakuna tena ruhusa ya kufunga. Hata hivyo, inaruhusiwa kufunga kwa yule mwenye ada ya kufunga Sunna za Jumatatu na Alhamisi kila wiki, au siku nyeupe kila mwezi.

Kwa wengine kuna katazo la kufunga baada ya nusu ya Shaaban kupita. Imepokewa hadith kutoka kwa Abi Huraira (Allah amridhie) kwamba mjumbe wa Allah amesema: "Itakapomalizika nusu ya Shaaban basi msifunge." [Tirmidhi).

Je, ni wangapi tunalijua fundisho hili? Basi tuwaidhike na tujiandae kufunga swaumu za Sunna katika siku hizi za mwanzo wa Shaaban ili mwezi usije ukavuka nusu huku hatujapata fadhila za kufunga katika mwezi huo.

Hata wale walioruhusiwa kufunga baada ya nusu ya Shaaban tujue na wao pia wamekatazwa kufunga zikibakia siku mbili au tatu kuingia mwezi wa Ramadhan, kwa ushahidi wa hadith iliyosimuliwa na Abi Huraira (Allah amridhie). Katika hadith hiyo, mjumbe wa Allah amesema: "Msiitangulie Ramadhan kwa swaumu ya siku moja au siku mbili, isipokuwa mtu aliyekuwa akifunga swaumu (za sunna) basi na afunge." [Bukhari na Muslim].

Zikiwa zimesalia wiki chache kabla ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan kuingia, tujitahidi kujikurubisha kwa Allah kwa kufanya ibada mbalimbali huku tukimuomba msamaha. Haipendezi na wala haitegemewi kwa Muislamu unapoingia mwezi wa Ramadhan kuwa kama mgeni.

Inapoingia Ramadhan tunatakiwa kuongeza kasi ya kumuabudu Allah Ta'ala na siyo kuanza. Tunamuomba Allah atuwafikishe kuufikia mwezi wa Ramadhan na atupe hima ya kuutumia ipasavyo.

# فتاوى رَجَب



**SHEIKH**
**Shaaban Mussa**
**0786 272 323**

## Swali: Wasia unaandikwaje?

**Jibu:** Binafsi sijui kuwepo kwa andiko maalumu linalobainisha namna mahsusi ya kuandika wasia. Hata hivyo, kidesturi wasia unapaswa kubainisha hali ya akili na mwili ya mwenye kuusia wakati wa kuandika wasia.

Ni vyema pia aeleze itikadi yake, kama kutaja shahada mbili au mfano wake, pamoja na kuwahimiza warithi wake kumcha Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Aidha, anapaswa kufafanua madeni anayodaiwa na watu wengine na pia madeni anayodai watu. Kadhalika, ataje aina na kiwango cha kitu alichokiachia wasia, kama nyumba au duka, na sehemu yake katika mali yake, kama theluthi au robo. Pia ateue msimamizi wa kusimamia wasia wake, mashahidi, na aeleze mahali au namna wasia huo utakavyotekelezwa.

Ikiwa ana watoto walio chini ya umri wa baleghe, inapendekezwa amteue msimamizi atakayesimamia malezi na maslahi yao hadi wafikie baleghe. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Swali: Ni ipi hukumu kuhusu mtu aliyochukua Msahafu kutoka msikitini, kisha akaweka badala yake kitabu cha tafsiri chenye maandishi ya Msahafu pamoja na tafsiri pembeni kwa sababu maandishi ya Msahafu aliyouchukua ni makubwa na rahisi kusoma, na tafsiri aliyoweka ni mpya na ya gharama kubwa? Msahafu aliouchukua amekuwa nao kwa muda wa miaka miwili. Je, anatakiwa afanye nini, na je, kitendo hiki kinaruhusiwa?

Jibu: Haijuzu kuhamisha Msahafu uliowekwa wakfu kwa ajili ya wasomaji katika msikiti na kuuchukua kwenda nao nyumbani. Wajibu wako ni kuurudisha Msahafu uliouchukua na kuupeleka mahali pake ili wasomaji waendelee kuusoma hapo. Haikubaliki kuubadilisha kwa kitabu kingine, iwe ni tafsiri au chochote kingine. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## Swali: Ni ipi hukumu ya dalali kuuza nyumba, ardhi au mali nyingine kwa bei ya juu kuliko ile aliyopangiwa na mmiliki?

**Jibu:** Hukumu hutegemea makubaliano kati ya mmiliki wa mali na dalali. Ikiwa mmiliki ameweka bei maalumu na akabainisha pia ujira wa dalali, dalali haruhusiwi kuchukua fedha ya ziada endapo atauza kwa bei ya juu. Fedha ya ziada ni haki ya mmiliki, na dalali anastahiki ujira waliokubaliana tu, kwa kuwa wakala ni mwaminifu na haruhusiwi kuvuka mipaka ya aliyoidhinishiwa.

Ikiwa mmiliki atasema wazi kuwa mali iuzwe kwa bei fulani na chochote kitakachozidi ni cha dalali, na dalali akakubali, muamala huo unaruhusiwa kisheria, na ongezeko la bei linakuwa halali kwa dalali kwa kuwa mmiliki ameridhia wazi. Kwa kifupi, dalali akichukua ziada bila idhini ya wazi ya mmiliki haijuzu, lakini mmiliki akiruhusu wazi ziada iwe ya dalali, inajuzu. Hii ni kwa sababu katika sheria ya Kiislamu, haki za mali lazima ziwe wazi na makubaliano yasiwe na mchanganyiko au udanganyifu. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## Swali: Ni yapi masharti ya sadaka endelevu (sadaka jariya)? Je, kuandika nyumba iwe ya mmoja wa ndugu au jamaa kunahesabika kuwa sadaka jariya, ikizingatiwa kuwa mwenye nyumba hana watoto na ndugu zake ni maskini?

**Jibu:** Sadaka jariya, kwa mujibu wa wanazuoni, inajulikana kama wakfu. Maana ya wakfu ni kufungia mali fulani isiuzwe wala isimilikiwe, huku manufaa yake yakitolewa kwa njia ya sadaka.

Wanazuoni wameeleza kuwa wakfu una masharti ya msingi ili uwe sahihi. Miongoni mwa masharti hayo ni kwamba mwenye kutoa wakfu awe mmiliki halali wa mali, awe na akili timamu na awe mtu mzima. Wakfu haukubaliwi kutoka kwa mtoto mdogo, mwendawazimu au mtu asiye na busara katika matumizi ya mali. Mali inayowekwa wakfu lazima iwe mali halisi, inayojulikana na inayoruhusiwa kisheria kuuzwa. Wakfu pia lazima uelekezwe katika jambo la kheri na utiifu kwa Allah, kwa kuwa ni ibada na sadaka.

Aidha, wakfu unapaswa kuelekezwa kwa anayejulikana au upande maalumu, kama msikiti au mtu fulani, lakini si kwa mwenye wakfu mwenyewe. Wakfu lazima ufanywe mara moja, bila kuufungamanisha na masharti ya baadaye, bila kuwekewa muda, wala hiari ya kuufuta. Masharti yanayopingana na maana ya wakfu, kama kudai haki ya kuuza au kuutoa baadaye, yanaharibu wakfu.

Kuhusu kuandika nyumba kwa ndugu au jamaa, ikiwa nyumba imeandikwa ili kumilikiwa moja kwa moja na ndugu au jamaa, basi inakuwa mali yake na hili ni zawadi, si sadaka jariya, ingawa mwenye kutoa atapata thawabu, InshaAllah. Lakini ikiwa nyumba imeandikwa kama wakfu, maana yake haiuzwi na manufaa yake hutolewa kwa huyo jamaa au katika njia za kheri, basi hiyo ni sadaka jariya halali, mradi itolewe papo hapo na mwenye kutoa awe mtu mzima, mwenye akili na hiari.

Tanbihi muhimu ni kwamba wakfu ukiunganishwa na kifo, yaani utekelezwe baada ya kufa, unahesabiwa kama wasia. Ikiwa wakfu huo umeelekezwa kwa warithi, hauwi halali isipokuwa warithi wengine wote wakubali, na wawe watu wazima, wenye akili na busara. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

HABARI

HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU




# Sekta ya benki ya Kiislamu yatabiriwa kukua kwa kasi nchini Malaysia

Sekta ya benki ya Kiislamu nchini Malaysia inatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi na kufikia karibu nusu ya thamani ya sekta nzima ya benki ifikapo mwaka 2030, kutoka asilimia 42 mwishoni mwa 2024.

Kwa mujibu wa The Borneo Post (Sarawak), ikirejea uchambuzi wa S&P Global Ratings kwenye ripoti yake "Asia-Pacific Islamic Banking Outlook 2026: Rebound Masks Regional Divergence", ukuaji huo unachangiwa na sababu anuai.

Sababu hizo ni pamoja na mfumo mpana wa usimamizi na kanuni, soko kubwa la sukuk la ndani, pamoja na kukubalika kwa huduma za benki za Kiislamu miongoni mwa wananchi na wafanyabiashara wadogo.

S&P imeeleza kuwa wateja wa rejareja na biashara ndogondogo wataendelea kuwa injini ya ukuaji wa sekta ya fedha ya Kiislamu, sambamba na mwenendo unaoonekana pia kwenye benki za kawaida.

Hata hivyo, ushindani mkubwa katika soko la Malaysia umefanya baadhi ya benki kubwa kuangalia fursa za kupanuka nje ya nchi, hususan Kusini Mashariki mwa Asia, ikiwemo huduma za usimamizi wa mali kwa mtindo wa Kiislamu.

Ripoti hiyo pia inaashiria ubora wa mikopo kuendelea kuwa mzuri Malaysia na Brunei, ikitabiriwa kuwa kiwango cha mikopo chechefu kitaendelea kuwa chini ya asilimia 2.0. Wachambuzi wanasema mwelekeo huu unaipa Malaysia nafasi ya kuendelea kuwa kitovu muhimu cha fedha za Kiislamu katika eneo la Asia-Pasifiki.

# Mughal wa AlHuda CIBE ateuliwa Mshauri wa Shariah wa fintech ya Nigeria


Muhammad Zubair Mughal

**LAGOS — Taasisi ya AlHuda Centre of Islamic Banking and Economics (AlHuda CIBE) imetangaza kuwa Mkurugenzi wake Mtendaji, Muhammad Zubair Mughal, ameteuliwa kuwa Mshauri wa Shariah wa Open Space Financial Services Limited, kampuni ya fintech na akili bandia ya Nigeria.**

**Mughal anaanza mara moja majukumu ya kutoa ushauri kuhusu mifumo ya usimamizi wa Shariah, taratibu za ufuataji wa kanuni, uthibitishaji wa bidhaa na kuhakikisha huduma za kifedha zisizo na riba za Open Space zinaendana na misingi ya kimataifa ya fedha za Kiislamu, matarajio ya wadhibiti na viwango vya uendeshaji vinavyokubalika kwa wawekezaji.**

**Taarifa inaeleza kuwa ushirikiano huo unaimarisha dhamira ya Open Space ya kujenga uendeshaji wa kimaadili na unaozingatia Shariah ndani ya shughuli zake za kifedha, sambamba na matumizi ya teknolojia ya kisasa.**

**Pia, uteuzi huo umetajwa kuonyesha kuongezeka kwa imani ya kimataifa katika uzoefu wa AlHuda CIBE kwenye masuala ya benki ya kimaadili, fedha za Kiislamu na mifumo ya huduma zisizo na riba.**

**Open Space inaendesha jukwaa la kidijitali linalotoa bidhaa zisizo na riba pamoja na huduma za kawaida kama akiba, uwekezaji, mikopo, bima na ufadhili wa bidhaa kwenye maghala. AlHuda CIBE ilieleza kuwa uteuzi huu ni sehemu ya upanuzi wake wa kimataifa katika ushauri wa kitaalamu, ikilenga kusukuma mbele mifumo ya fedha iliyo wazi, jumuishi na yenye uwajibikaji.**

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 1

Na Said Rajab

0783 650 803

# Kauli ya 'Mtoto ni mali ya jamii nzima' imefia wapi?

**Tulipokuwa watoto kulikuwa na msemo kuhusu malezi uliosema, mtoto ni wa jamii nzima, siyo tu wazazi wake. Hivi msimamo huu wa malezi ya watoto umeenda wapi siku hizi? Suala la malezi limekuwa jambo binafsi na limeachwa kwenye 'screen' za kompyuta, simu, na vifaa vingine vya kielektroniki.**



# Kauli ya 'Mtoto ni mali ya jamii nzima' imefia wapi?

Tulipokuwa watoto kulikuwa na msemo kuhusu malezi uliosema, mtoto ni wa jamii nzima, siyo tu wazazi wake. Hivi msimamo huu wa malezi ya watoto umeenda wapi siku hizi? Suala la malezi limekuwa jambo binafsi na limeachwa kwenye 'screen' za kompyuta, simu, na vifaa vingine vya kielektroniki.

Wengi wetu siku hizi tunalea watoto peke yetu kimwili, kihisia na hata kidijitali. Malezi ya jamii yameondoka, simu janja zimechukua nafasi yake, na watoto wetu wanalipa gharama hiyo. Enzi hizo tulipokuwa tunakua hatukuchungwa na mama na baba peke yao bali tulichungwa na mashangazi, mama wadogo, wajomba, mabibi, mababu, majirani na hata wauza maduka mtaani. Wote hawa walikuwa na nafasi ya kutulea.

Mmojawapo lazima angetambua iwapo ungekuwa unatoka nje ya mstari. Mmojawapo lazima angekuwa na muda wa kuzungumza nawe, kukuonya au hata kukubusu. Kwa masikitiko makubwa, mtandao wote huo wa malezi leo umesambaratika kabisa. Ukuaji wa miji umezitawanya familia katika miji na mabara yote.

Shinikizo la kiuchumi linasababisha wazazi hufanya kazi kwa saa nyingi zaidi au kufanya kazi nyingi kwa pamoja. Mzazi mmoja mmoja hubeba mzigo wote. Mara nyingi bibi na babu huwa mbali. Matokeo yake, watoto wengi sasa humtegemea mtu mzima mmoja au wawili tu na wakati mwingine mzazi mmoja (single parent) kwa kila kitu, kuanzia chakula, usafiri, usaidizi wa kihisia, mipaka, na muongozo wa kimaadili.

Watu wazima hao wanapochoka, kufadhaika, au kutokuwepo, watoto huwageukia wenzao, na mara nyingi zaidi 'screen' zao za kompyuta, simu, televisheni au vifaa vingine vya kielektroniki ili kupata majibu.

Mtaalamu wa elimu, Sue Palmer, anahoji katika kitabu chake mashuhuri 'Toxic Childhood' kwamba, mmomonyoko wa familia thabiti na maisha ya jamii umewaacha watoto bila mifano mingi ya watu wazima (role models), inayowasaidia kukuza ustahimilivu, nidhamu na huruma.

Bila ya mfumo huo wa malezi ya kijamii, ambao ulikuwepo awali lakini tumeupuuza, hakuna mtu wa kuona dalili za kuchukuliwa tahadhari mapema, au kutoa muongozo nje ya mfumo wa mzazi na mtoto. Na si watoto pekee wanaoteseka, wazazi pia wanahangaika.

Bila ndugu, jamaa au majirani kushiriki katika kubeba mzigo huo, wazazi hawatoweza kupumzika, hawatopata nafasi ya kupumua wala kuzungumza na watu wazima wenzao. Haishangazi wazazi wengi wanaripoti uchovu, au kwamba viwango vya msongo wa mawazo na mfadhaiko vimeongezeka.

## Teknolojia ndiyo mlezi mpya wa watoto

Ikiwa mfumo wa malezi uliopotea ni nusu ya hadithi, basi kuibuka kwa teknolojia ni nusu nyingine ili kukamilisha hadithi hii. Tunawapa watoto vifaa ili kuwanyamazisha, kisha tunageukia 'screen' zetu wenyewe ili kukabiliana na hali hiyo. Lakini hii ina gharama zake.

Watafiti wanaiita hali hii "technoforence" – yaani wazazi wanakengeushwa na vifaa vya kielektroniki katika muda wa kukaa na familia zao. Utafiti umegundua kwamba watoto ambao wazazi wao mara nyingi hutumia simu au kompyuta mpakato (laptops), huwa na wasiwasi zaidi, matatizo mengi ya tabia na hisia dhaifu ya usalama.

Lakini pia kuna kinachotokea kwenye 'screen' za watoto wenyewe. Mitandao ya kijamii hubadilisha michezo ya kompyuta kuwa kipindi cha uhalisia (reality show) kinachoendelea saa 24. Unyanyasaji wa mtandaoni huwafuata watoto vyumbani mwao. Mitandao hii huwalisha watoto maudhui ambayo hawako tayari kuyabeba kihisia.

Usingizi, umakini na kujithamini huathirika. Sue Palmer alionya takriban miongo miwili iliyopita kwamba, kuwaachia sana watoto vifaa vya kielektroniki (screen saturation) kunadhoofisha ujuzi wao wa lugha, ukuaji wao wa kihisia, na uwezo wao wa kucheza nje. Leo hii onyo lake limekuwa halisi.

## Gharama tunayolipa

Bila mfumo na uwepo wa teknolojia nyingi, tuna hatari ya kukuza kizazi kisicho imara, kisicho na uhusiano wa karibu, na kisicho na msingi madhubuti. Watoto hutegemea zaidi wenzao na utamaduni wa rika, ambao mara nyingine si mzuri. Wazazi huchoka sana, hali inayosababisha ukali katika kujenga nidhamu au kujiondoa kihisia katika malezi.

Jamii zinadhoofika huku familia zikiishi maisha ya kujifungia ndani. Shirika la Afya Duniani (WHO) tayari limetambua kutengwa kijamii (social isolation) kama hatari kwa afya ya umma. Kutengwa huko huanzia kipindi cha utotoni. Nini cha kufanya kurekebisha hali hii. Tukutane katika toleo lijalo Insha Allah!



رَجَب

MAKALA MAALUM

0712 690 811



NA SHEIKH SEIF RUGA

SEHEMU YA 1

# Misingi ya kuasisi ndoa imara katika Uislamu

**Msingi wa maisha ya ndoa katika Uislamu ni upendo, kaulimbiu yake ni huruma na maelewano. Maisha ya ndoa katika Uislamu siyo tu kuizuia nafsi na tamaa ya mwili, wala si starehe pekee; bali ni jambo kubwa zaidi kuliko hayo.**

**Ni hisia za kubadilishana mawazo yaliyoundwa na uhusiano wa karibu na upendo wa kina wa pande zote, kushirikiana katika kubadilishana furaha na huzuni, na kushirikiana katika vyanzo vya furaha na sababu za faraja.**

**Taswira hizi zimeelezwa wazi katika Qur'an Tukufu pale Allah aliposema: "Na miongoni mwa ishara zake (Mwenyezi Mungu) ni kwamba amekuumbieni wake zenu kutoka katika nafsi zenu ili mpate kutulia kwao, na amejaalia baina yenu mapenzi na huruma. Hakika katika hayo zipo ishara kwa watu wanaotafakari." [Qur'an, 30:21].**

Uislamu umeipa ndoa uangalizi mkubwa na umakini wa hali ya juu, kwa kutambua kwamba uadilifu wa ndoa humaanisha uadilifu wa jamii ya Kiislamu. Ndiyo maana Qur'an Tukufu imeeleza hukumu za ndoa na familia, na yanayohusiana nayo katika Aya 146. Huu ni ushahidi mkubwa na muhimu katika suala hili.

Vilevile, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ametoa muongozo unaoleta furaha na neema. Hata hivyo, uhusiano huu wa kisharia na ahadi nzito (miithaq ghalidh) unaweza kukabiliwa na matatizo mengi ya kindoa na kifamilia yanayokwamisha maendeleo.

Kwa kuzingatia hilo, ndiyo maana Mtume wa Allah amesema: "Atakapokujieni mnayeridhia dini na tabia yake muozesheni; msipofanya hivyo kutakuwa na fitina katika ardhi na uharibifu mkubwa." [Tirmidhi]. Na kauli yake Mtume: "Mbora wenu ni yule aliye bora zaidi kwa watu wa nyumbani mwake, na mimi ni mbora wenu kwa watu wa nyumbani kwangu." [Tirmidhi].

Hadith hizi za Mtume (rehema na amani zimshukie) zimeweka msingi imara katika uhusiano wa kindoa, kuanzia katika kuchagua mchumba na kuishia kwenye ridhaa na kukubaliana kunakodhihirishwa na wema na ubora wa tabia.

Kwa msingi huo, jambo muhimu na la lazima katika maisha ya kila mmoja wetu, na kwa lengo la kuzuia matatizo katika maisha ya ndoa, ni kuchunguza kwa makini na kwa weledi mkubwa mchakato mzima wa kumpata mchumba.

Kuchagua mwenza wa maisha, kama hatua ya kwanza katika maandalizi ya ndoa, ni miongoni mwa maamuzi muhimu na hatarishi zaidi katika maisha ya mwanaume na mwanamke. Ni hatua ya kuamua usalama wa ndoa, kudumu kwake, furaha yake, kuyumba kwake, kuvunjika kwake na taabu zake.

Familia ni nguzo ya jamii, na ndiyo kiini cha kwanza katika ujenzi wake. Kadri familia inavyokuwa imeshikamana na kushirikiana ndivyo jamii inavyokuwa imara. Msingi wa ushirikiano kati ya wanafamilia ni upendo na heshima ya pande zote, na mapenzi haya hayapatikani ila kwa kuchagua mwenza wa maisha kwa umakini na kumcha Allah katika jambo hilo.

Iwapo kila mmoja wa wanandoa atamchagua mwenzake kwa uangalifu na akamcha Allah katika namna ya kuamiliana naye, basi Allah Mtukufu atawaneemesha kwa upendo na maelewano. Hata hivyo, kuwepo kwa mapenzi na maelewano haimaanishi hakuna tofauti na migogoro ya kindoa, wala maisha yasiyokuwa na changamoto.

Hili ni jambo la kawaida katika maumbile ya mwanadamu, ndiyo maana hata Manabii na Mitume wa Allah hawakusalimika na hali hiyo. Imepokelewa katika Sunna kwamba Mtume wa Allah aliwahi kujitenga na wakeze kwa muda wa mwezi mmoja, kisha akawapa hiari ya kurejea au kuachana.

Kwa sasa tunaishi katika mabadiliko makubwa yanayotokana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kitamaduni. Zamani, jukumu la kuchagua mwenza wa maisha lilikuwa linafanywa zaidi na mama au wanawake kwa ujumla (wazazi), na kijana aliyekuwa anakusudia kuoa au kuolewa hakuwa na nafasi kubwa ya kushiriki katika uamuzi au kuchagua mchumba yeye mwenyewe.

Lakini leo hali imebadilika; jukumu hili limekuwa likifanywa moja kwa moja na mvulana au msichana mwenyewe kwa juhudi zao binafsi, bila kushauriana na wazazi wao au kutafuta msaada wao kwa matumaini ya kufikia maelewano makubwa zaidi katika maisha yao ya ndoa.

Kuchagua mwenza wa maisha kwa wanaotaraji kuingia kwenye ndoa ni msingi ambao juu yake kunajengwa maisha ya ndoa yaliyo salama, thabiti na yasiyo na matatizo. Kwa kuwa ndoa inasimama juu ya miunganiko miwili mikuu, ambayo ni muungano wa kisharia na muungano wa kiroho, basi muungano wa kisharia na utekelezaji wa mkataba hauhitaji zaidi ya kutimia kwa masharti ya kisharia yanayohitajika ili mkataba wa ndoa uwe sahihi.

Hata hivyo, muungano huu pekee hauhakikishi maisha ya ndoa yaliyo na usawa na utulivu. Ama upendo unaozaliwa kutokana na mvuto na maelewano kati ya jinsia mbili, hujenga muungano wa kiroho wenye msingi imara unaosaidia kuendelea na kudumu kwa maisha ya ndoa kati ya mume na mke.

*Itaendelea katika toleo lijalo Insha Allah*

رَجَب

NASAHA
ZA WIKI
0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Kutokinai kunavyowatesa vijana kimyakimya

**Katika zama hizi, watu wengi, hususan vijana wanaamini utajiri ni kumiliki mali au pesa nyingi. Dhana hii imetawala mawazo yao na imekuwa ikijibainisha katika maisha yao ya kila siku, wakiamini furaha ya kweli na amani ya nafsi (peace of mind) vitapatikana kwa wao kumiliki mali yingi.**

Hata hivyo, ndugu yangu unayesoma makala hii, elewa kwamba maisha 'mazuri' unayoyatamani hayatokusaidia kitu mbele ya Allah. Qur'an yatuambia: "Mali na watoto ni pambo la uhai wa dunia. Na mema yanayobakia ni bora mbele ya Mola wako kwa thawabu na matumaini." [Qur'an, 18:46].

Utambuzi huu ukuelekeze katika kufahamu kuwa, kukinai ndiyo msingi wa utulivu, raha na amani ya nafsi na siyo utajiri. Hakuna kitakachofanya uishi kwa furaha na utulivu hapa duniani isipokuwa kukinai na kuridhia kwa kile alichokukadiria Allah.

Imepokewa hadith kutoka kwa Sahl bin Sa'ad (Allah amridhie) akieleza kuwa, mtu mmoja alikuja kwa Mtume (rehema za Mwenyezi Mungu na amani iwe juu yake) akamwambia: "Ewe Mtume wa Allah! Nijulishe amali ambayo nikiifanya Allah atanipenda na watu pia watanipenda." (Mtume) akamwambia: "Ipe mgongo dunia Allah atakupenda, na vipe mgongo vilivyo kwa watu, watu watakupenda." [Ibn Majah].

Hadith hii inawiana kimaana na methali ya Kiswahili isemayo "Kisicho chako usikitegemee." Maana yake usitamani kumiliki kitu kisichokuwa chako. Hivyo basi, kimsingi methali hii inatufundisha kuridhika na makadirio ya Allah, pamoja na kutambua hali na mabadiliko ya maisha ya kidunia na hakika yake.

Ni kwa kuzingatia hilo, utakuta Aya nyingi ambazo zinayaponda maisha ya dunia mara nyingi huishia kwa kutaja na kukumbusha neema za maisha ya Akhera. Hii ni ishara ya kuonesha namna imani ilivyo na nguvu na taathira kubwa ya kurithisha tabia ya kukinai katika nyoyo na kuipa nyongo dunia.

Muumini ambaye itikadi yake imesafika na kusalimika na kile kilichohukumiwa na kukadiriwa na Allah kitokee, hutomuona isipokuwa katika hali ya kuridhika na kila alichowepesishiwa na Allah katika maisha. Muumini huyu utamkuta amekinai na kuridhika na hali yake, kama alivyosema Mtume (rehema na amani imshukie): "Ridhika na kile alichokugawia Allah utakuwa tajiri wa watu." [Ahmad].

Siri iliyopo katika ufahamu sahihi wa itikadi ya Qadar ni kuwa, inamfanya mtu awe ni mwenye kukinai kwa sababu ya kutambua kuwa Allah amekwishagawanya riziki kwa waja wake na hakuna atakayechuma isipokuwa kile alichokadiriwa.

Pia, mja atafahamu kuwa Allah ndiye anayewaweka watu katika madaraja tofauti kwa elimu yake na hekima yake, na amefanya hivyo ili maisha ya viumbe yaweze kuendelea, kwani kila mmoja anamhitajia ndugu yake katika mambo asiyoweza kumudu kuyafanya katika maisha yake.

Mwenyezi Mungu anasema: "...sisi tumegawanya baina yao maisha yao katika uhai wa duniani, na tukawanyanyua baadhi yao juu ya wengine kwa daraja nyingi; kwa hivyo baadhi yao wanawafanya wengine wawatumikie. Na rehema za Mwenyezi Mungu ni bora kuliko hayo wanayoyakusanya." [Qur'an, 43:32].

Katika Aya hii, Allah anatueleza hekima ya kutofautisha watu katika maisha yao na vipato vyao. Muumini anatakiwa atambue kwamba, kuwa na pupa, tamaa na kuiweka dunia mbele ya macho kwa kuifanya kuwa ndiyo kila kitu hakutamfaidisha chochote; si kupata ziada ya riziki yake, wala kupunguza matatizo yake, wala kubadilisha maamuzi ya Allah, hukumu yake na makadirio yake.

Tofauti zetu za kimaisha ni mtihani baina yetu, ni mtihani kwa tajiri anapozidishiwa, vilevile ni mtihani kwa masikini anapopunguziwa. Kamwe tofauti hizi si dalili ya ubora wa mmoja kati yetu. Kufadhilishwa katika mali si dalili ya kupendwa na Allah; na kukosa kipato cha kutosheleza si dalili ya kuchukiwa na Allah.

Hata hivyo, maandiko mengi katika Kitabu cha Allah na Sunna za Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) yanaonesha kuwa umasikini una usalama zaidi kwa muumini kuliko utajiri.

Kwa hiyo, kwa hali zote mbili, kukinai ni hatua muhimu sana katika maisha ya Muislamu na inampa utulivu kwa hali yoyote atakayokuwa nayo. Muislamu anahitaji kumuomba Allah amruzuku tabia ya kukinai kuliko anavyomuomba mali na cheo.

## Vumilia, pambana na nafsi

Kwa kawaida nafsi humpa mtu msukumo wa kuasi na humpambia matamanio. Ukitazama tabia ya kukinai, utaona iko mbali kabisa na mtu mwenye tamaa na matamanio ya kilimwengu. Mtu asipofanya juhudi ya kupambana na matamanio ya nafsi yake atakuwa anajifungulia mlango wa pupa, tamaa, ubahili na uchoyo. Hizi ni tabia mbaya zinazoangamiza watu wengi na kuwanyima utulivu katika maisha yao.

Mwenyezi Mungu anasema: "Na ama yule anayeogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi, na akajizuilia nafsi yake na matamanio, basi huyo Pepo itakuwa ndiyo makazi yake!" [Qur'an, 79:40–41]. Kupambana na ukaidi wa nafsi na kuifanya ikinai kunahitaji uvumilivu, kwani nafsi ya mwanadamu imeegemea zaidi katika kupenda mambo ya maasi na matamanio ya kidunia.

Ukweli mchungu ni kwamba, watu wengi hasa vijana wametumbukia kwenye maasi na mambo ya pumbao kiasi cha kumfanya yule mwenye kukinai kuonekana ni mgeni katikati ya watu. Tatizo kubwa linaloonekana wazi kwa vijana wengi ni kufanya mambo kwa mazoea au kwa kuiga wengine.

Hii ina maana, yule ambaye muda wake mwingi atakuwa anautumia pamoja na watu wenye tamaa na matamanio, watamuathiri kwa tabia zao na atakuwa si mwenye kukinai. Kinyume chake ni kwamba, kufuatana na watu wema ni sababu ya kuathirika na tabia zao njema.

MUSSA IMANI SHEHA, ZANZIBAR

# Ujumbe kwa Wasomi Waislam

**Uislamu ni dini ya elimu, na imepiga vita ujinga tokea mwanzo wa risala (ujumbe) yake kwa walimwengu. Aidha, Uislamu umehimiza kusoma elimu zote zenye manufaa kwa mwanadamu.**
**Uislamu hautenganishi elimudini na elimudunia. Kila elimu ina nafasi yake katika maisha ya mwanadamu alimradi iwe kwa ajili ya Muumba. Na mtaalamu wa fani yoyote ni hitajio la jamii inayomzunguka kwa ustawi wake.**
**Lakini kuna elimu ya msingi na ambayo kila Muislamu anapaswa kuijua, nayo ni elimu ya dini, ambayo ndio muhimili na msingi wa elimu zote.**
**Hii ni elimu ya kumtambua Allah Muumba na ulazima wa kumtumikia. Elimu ya kumjuvya mwanadamu haki na majukumu yake kwa viumbe wenzake kiimani, na kumuongoza kuwa na tabia njema, na kujali shida za wengine.**

## Hali ya jamii

Jamii leo inaonekana kuvutika sana na elimu ya mazingira ama "elimuajira." Juhudi wanazozifanya wazazi za kuhakikisha watoto wao wanaipata elimu ya mazingira hatimae kupata ajira ni kubwa sana, na huanza mapema kabisa. Hupitia ngazi zote: maandalizi, msingi, sekondari hadi chuo.

Lakini kwa upande wa masomo ya dini, juhudi hizi hazionekani sana - si kwa wazazi wala kwa hao watoto na vijana wenyewe waliokwisha kuisoma picha na kujua nini haswa wanachokihitajia wazazi wao.

## Matokeo yake

Matokeo ya upuuzaji huu mkubwa wa elimu ya kiroho ni kuwa na idadi kubwa ya wasomi Waislamu, bobezi katika fani mbali mbali katika elimu ya mazingira lakini wana uelewa mdogo sana kuhusu dini yao.

Aghlab, mambo huharibika na haki za watu kupotea pale wasomi hao wanapopewa dhamana ya kuwa viongozi na watumishi wa umma kama wanasiasa, madaktari, walimu, viongozi wa umma, askari, walinzi, wanahabari, mahakimu, wanasheria, mawakili nk.

Utashi na tamaa za kujipatia maslahi, huushinda utu, huruma na kujali shida za watu. Uzembe, utapeli, rushwa, majungu na hata ushirikina kazini, uongo, na hiyana: huwatawala wasomi hao.

Pia, hawasalimiki na wizi wa mali ya umma pale wanapoamini kuwa hakuna jicho la mtu au chombo cha sheria kinachowamulika . Jamii yenye wasomi na watendaji kama hao hujikuta inanyonywa na kubeba mzigo mzito usio na faida kwake, na maisha ya wanajamii kuwa magumu zaidi.

Upuuzaji wa maagizo ya Allah –kama vile swala- kwa wasomi hao ni kitu cha kawaida. Baadhi yao hufikia hatua ya kuwadharau waliosoma dini, wakajawa na kibri na kutoa lugha za kejeli dhidi ya Uislamu (dini yao wenyewe) na viongozi wake.

Wasomi hao hujiliwaza: eti kwa vile wamesoma sana fani zao mbali mbali, basi hata dini nayo wanaijua, na wana uwezo wa kuisemea wakitaka wakitegemea mantiki badala ya Qur'an na Sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia.

## Kuathirika na umagharibi

Mtihani zaidi ni wasomi hao kuathiriwa na nadharia za wasio Waislamu (hasa ulimwengu wa kimagharibi) wakawapenda na kuwasifia kuliko Waislamu wenzao.

Huzimeza historia, tafiti na nukuu za watafiti na vumbuzi zao, lakini wanashindwa kujua historia ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) na Maswahaba wake (Allah awaridhie), wala hawawezi kunukuu aya, hadith au kauli za wataalamu (wasomi) wa Kiislamu.

Tazama ndugu zetu hawa –Allah atuongoze sisi na wao-wanavyokuwa wageni siku zote katika utekelezaji wa ibada misikitini. Naam, kwa sababu hawajifunzi na wala hawana mpango wa kujifunza!

Pitia darsa za misikitini, mihadhara ya dini pamoja na taasisi za maarifa ya Uislamu, halafu angalia washiriki wa programu hizo ni akina nani? Hatutarajii kwamba, utawaona wengi katika waitwao wasomi na ambao wana ajira (nyadhifa) zao kubwa kubwa au wenye vipato vikubwa (matajiri).

Haitarajiwi pale kuwakuta: wakurugenzi, makatibu wakuu, wabunge, mawaziri, maafisa, mameneja, wakuu wa mikoa na wilaya nk. ambao ni waislamu, ambao walipaswa pia kujifunza na kuijua vyema dini yao!!

## Wito

Tunatoa wito kwa wazazi kuwapeleka watoto wao katika taasisi za elimu ya dini (madrasa na ma'had) wakajifunze imani iwasaidie katika kujenga mahusiano mema na Mola wao, na kuwa raia wema wasiwe mzigo kwa wanajamii wenzao.

Tunawaambia ndugu zetu waliosoma elimu ya mazingira (sekula) na kushika nyadhifa mbali mbali, na ambao hawakubahatika kuijua dini yao: bado hawajachelewa.

Muda bado upo na wajibu uko pale pale. Wajishuhulishe na kuisoma dini yao kwa namna majukumu yatakavyowaruhusu. Kuweni karibu na wasomi wa dini mubadilishane uelewa kwani elimu ni bahari.

Saidianeni katika kuwaongoza watu njia iliyo sahihi. Jamii inawategemea sana, ioneeni huruma. "Mbora wa watu ni awatumikiae watu."

JUNAYNAT ALLY DAMA



# Haya yanakufanya ufurahie au uyachukie mazoezi ya kukimbia

Utafiti mpya uliofanyika jijini Vancouver, Canada, umejaribu kujibu swali ambalo wakimbiaji wengi hujiuliza kimya kimya: kwa nini siku moja kukimbia kunahisi kuzuri sana, lakini siku nyingine kunachosha na kukera?

Tofauti na tafiti nyingi zinazopima umbali, muda au kasi pekee, utafiti huu ulitumia simulizi halisi za wakimbiaji waliandika hisia zao baada ya kukimbia kwenye programu ya Strava.

Kwa kuchambua maelfu ya maelezo ya wakimbiaji, watafiti walibaini kuwa uzoefu wa kukimbia hauamuliwi na nguvu za mwili pekee, bali na mchanganyiko wa mazingira, hali ya hewa, watu, njia, hali ya mwili na msukumo wa kisaikolojia.

Matokeo haya yana umuhimu mkubwa kwa Tanzania, ambako vilabu vya wakimbiaji (jogging) vinaongezeka kwa kasi katika miji kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma. Makundi haya yamekuwa yakihamasisha afya, umoja na mtindo bora wa maisha.

Hata hivyo, changamoto imebaki ile ile: watu wengi huanza kwa hamasa kubwa, lakini hawadumu. Wengine huacha kimya kimya wakisema "mbio zimenishinda" au "sifurahii tena."

Utafiti huu unatoa mwanga muhimu kwa vilabu vya jogging na waandaaji wa mazoezi kuhusu nini hufanya watu wafurahie kukimbia na nini huwafanya wachukie na hatimaye kuacha.

## Hali ya hewa

Hali ya hewa ndiyo sababu inayojitokeza sana kwenye maelezo ya wakimbiaji. Wakimbiaji wengi hufurahia baridi ya wastani, upepo mwepesi na anga tulivu, kwa sababu mwili hauchoki mapema na pumzi inakuwa rahisi.

Kinyume chake, joto kali, unyevunyevu, mvua kubwa au upepo mkali vinaweza kufanya mwili ujisikie mzito, viatu kuteleza, na mhemko kushuka. Utafiti huo pia unaonyesha kuwa baadhi ya "trail runners" hupenda hali ngumu (baridi, upepo, mvua) kwa sababu inawapa ladha ya "changamoto na adventure," lakini kwa wakimbiaji wa barabarani, baridi kali au barafu huwa hatari na hufanya wachukie zaidi.

## Mazingira unayokimbilia

Mandhari yana nguvu ya kubadili hisia. Kukimbia kwenye maeneo ya kijani kama bustani na njia za miti, au karibu na maji, huongeza utulivu na "feel-good" kwa wakimbiaji wengi. Lakini mazingira yenye kelele, vumbi, harufu mbaya, au eneo linalohisi si salama huua hamasa.

Mwanga (illumination) pia ni kigezo: sehemu zenye giza au zisizo na watu wengi huongeza hofu na kufanya mazoezi ya kukimbia yataliwe na wasiwasi badala ya burudani.

## Njia ya kukimbia

Wakimbiaji wengi hupenda njia laini, zilizotunzwa, zenye mtego mzuri wa viatu na zisizolazimisha kusimama kila dakika. Sababu ni moja: kukimbia kunapokuwa na mwendelezo, mwili unaingia kwenye mtiririko mzuri (rhythm) na akili inapata utulivu.

Lakini ukikumbana na vikwazo vingi—barabara za kuvuka mara kwa mara, taa nyingi za kusimama, mashimo, changarawe inayoteleza, au msongamano wa watembea kwa miguu—kukimbia kunageuka kero.

Utafiti huo haukuonyesha "upendeleo wa pamoja" kuhusu kupanda milima; wengine hupenda changamoto na mandhari, wengine huichukia kwa sababu huongeza uchovu.

## Uzoefu wa mwili

Kuna tofauti kati ya "uchovu wa kawaida" unaojenga stamina na maumivu yanayoashiria jeraha. Wakimbiaji wengi huweza kuvumilia kukaza kwa misuli au uchovu wa kawaida, lakini maumivu ya jeraha, kuumwa viungo, au kujisikia mgonjwa hufanya uzoefu wa kukimbia uwe mbaya na hata kuvunja ratiba ya mazoezi.

Pia, watu wengi hupata ugumu mwanzoni mwa kukimbia: dakika za kwanza zinaweza kuhisi nzito kabla mwili haujapata "mwendo." Hili ni jambo la kawaida kisaikolojia na kifizikia kwa sababu mifumo ya mwili inahitaji muda kujibadili kutoka hali ya kupumzika kwenda kazi.

## Watu unaokutana nao na hali ya usalama

Mbio zinaweza kuharibiwa na tabia za watu wengine. Ustaarabu wa njia—waendesha baiskeli, watembea kwa miguu, au wakimbiaji wenzako kuheshimiana—huongeza furaha.

Msongamano, ukorofi, au kuhisi kutishiwa huleta hasira na kufanya mtu achukie kukimbia. Kwa upande mwingine, kukimbia na rafiki au kikundi kunaweza kuongeza hamasa na kufanya uhisi mbio ziwe nyepesi, ingawa bado wapo wanaopenda kukimbia peke yao kwa "personal time."




## MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Sikumjua aliye mbali na msikiti zaidi yake

**Imepokewa hadith kutoka kwa Ubayy bin Ka'b (Allah amridhie) akisema: "Alikuwepo mtu mmoja katika Answar, na sikumjua yeyote aliye mbali zaidi na msikiti kuliko yeye. (Mtu huyo) hakukosa sala (ya jamaa) hata moja, akashauriwa anunue punda wa kumpanda wakati wa giza (la usiku) na wakati wa joto kali. Mtu yule akasema: "Sifurahishwi nyumba yangu iwe karibu na msikiti. Mimi nataka niandikiwe (thawabu) za hatua zangu za kwenda msikitini na ninaporejea kwa watu wa nyumbani kwangu." Mtume (rehema na amani zimshukie) akasema: "Hakika Allah amekukusanyia hayo yote." *[Imepokewa na Muslim]***

## Mafundisho ya tukio hili

Kuimarisha nafsi katika utiifu na kudumisha kutekeleza mambo ya wajibu katika mazingira yoyote yale ni miongoni mwa matendo bora zaidi kwa Muislamu. Nafsi ya mwanadamu huchoka na kuzembea katika kumtii Allah hivyo huhitaji utakasifu unaosababishwa na mapambano ya mja baina yake na nafsi yake katika kuiteza nguvu na kuilekeza katika twaa.

Imani ya mja haikamiliki sawasawa ila kwa subira na kuizuia nafsi isiteleze katika mambo ya haramu, na kuwa na bidii katika yale ambayo nafsi inayaona kuwa ni mazito. Wenye hekima wamesema: "Nafsi ni kama mtoto, usipomzuia (kunyonya), atakua huku akiwa anapenda kunyonya; na ukimnyima (ukaacha kumnyonyesha) ataacha."

Mja anapovumilia, akadumu katika utekelezaji wa maamrisho ya Allah kwa namna yake sahihi, akaizuia nafsi yake kufanya maovu huku akipambana na yale magumu yanayoweza kuitia uzito nafsi, hujiona mtulivu na mwenye faraja moyoni, na huona mambo mazito kuwa ni mepesi.

Mja wa aina hii huyachukia maasi, hatimaye huonja ladha ya ibada na kuyaona mepesi mambo ambayo watu wengine wanaona kuwa ni magumu. Mwenyezi Mungu anasema: "Lakini Allah amekupendezesheeni imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na akakuchukizeni ukafiri, ufasiki na uasi. Hao ndiyo walioongoka sawasawa." [Qur'an, 49:7].

Mhusika wa tukio hili anawakilisha kizazi kitukufu kilichoimarishwa na mafunzo ya Uislamu. Unaloliona zito kwako katika kuufanyia kazi Uislamu, kwao lilikuwa jepesi mno. Umma wetu hivi sasa unahitaji watu wanaotambua kuwa wao ni matofali madhubuti katika kuimarisha jengo la umma.

Hii ni kwa sababu, kuharibika kwa umma kunatokana na kuharibika kwa watu wake; na kutengamaa au kuimarika kwa umma ni kule kuimarika kwa watu wake. Allah Mtukufu amekisifia kizazi bora kilichowahi kuishi katika umma huu ndani ya karne zinazosifika kwa kila aina ya ubora, kizazi kilichojua kwa uhakika wake maana ya tamko la 'Lailaha illaLlah; Muhammadu rrasuluLlah'.

Wao walifanyia kazi yale yote yaliyomo kwenye tamko hili na siyo kulitamka tu kwenye ndimi zao. Tamko hili halikuwa jepesi na la mpito kwao kama ilivyo kwa Waislamu wengi wa sasa, ambao hulitamka kwa wingi huku uhalisia wa maisha yao ukiwa kinyume kabisa na matakwa ya tamko hili.

Ndiyo maana Allah amekisifia kizazi hiki bora kilichoishi katika karne bora kwa kusema: "Nyinyi mmekuwa umma bora kabisa uliotolewa (mfano) kwa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu..." [Qur'an, 3:110].

Hii ni kwa sababu, wao walilitambua neno hili na wakalipa haki yake inayostahiki, waliunda jamii ya kiimani yenye haiba yenye nguvu, hatimaye ukapatikana umma uliosimama katika misingi ya imani moja ya kumtakasia ibada Allah peke yake na kumfuata Mtume ipasavyo.

Jamii hii ilitosheka na kumfanya Mtume (rehma za Allah na amani zimshukie) kuwa ndiye kigezo chao na kiongozi wao katika kila kitu, jambo ambalo liliwafanya wapandishwe daraja kubwa ya kupewa uongozi na mamlaka katika ardhi. Hiyo ndiyo ahadi ya Allah kwa wale watakaopita njia ya sawasawa katika imani na kutenda yaliyo mema.

"Allah amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya Makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya Makhalifa waliokuwa kabla yao. Na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya hofu yao, wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndiyo wapotovu." [Qur' an, 24:55].

Hivyo, kinachotakiwa ni kuziimarisha nafsi zetu ili tuwe na umma mmoja uliojengeka katika misingi ileile ya mwanzo, jambo litakalotupandisha daraja na kurejea katika nafasi yetu ya kuwa umma bora. Sahaba tunayemzungumzia katika tukio hili hakuwahi kukosa sala ya jamaa, lakini Muislamu wa leo anaweza akakosa kusali jamaa msikitini ilihali msikiti upo jirani kabisa na nyumba yake.

## Pande mbili za nafsi

Tukitazama mafundisho ya Uislamu, tunakuta nafsi ina pande kuu mbili. Upande wa kwanza ni ule wa maumbile ya asili, uliosalimika, na wenye kumtambua Allah, umeumbwa katika kupenda haki na kheri, na umewekewa maandalizi ya kuitambua haki na kuifurahia, na inasikitika pale inapokwenda kinyume na haki.

Lau kama si kuwapo kwa mvutano na upinzani, basi nafsi ingebakia katika asili yake, watu wote wangesimama katika mstari ulionyooka kimatendo na kitabia. Haya ni maarifa ya kimaumbile ambayo Allah ameyaweka kwenye nafsi na yanamsaidia mtu kuitofautisha haki na batili.

Upande wa pili wa nafsi unapingana na upande mzuri wa kimaumbile, ambao hudhoofisha na kuugeuza katika mila za kufru na shirk kutokana na ushawishi, udanganyifu na mambo mbalimbali, yakiwamo mazingira anayokulia mwanadamu tangu akiwa mtoto.

Katika hadithil Qudsy, Allah Mtukufu anasema: "Hakika mimi nimewaumba waja wangu wote wakiwa katika mila iliyo sawa, na hakika wao shetani aliwajia akawapondosha katika dini yao na akawaharamishia waliyohalalishiwa na akawaamrisha wanishirikishe kwa yale ambayo sijayateremshia ushahidi." [Muslim].

IDARA YA DAAWA

# Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

www.islamicftz.org




JUNAYNAT ALLY DAMA

# Tunavyoweza kutumia mitandao kuimarisha undugu

**Katika zama hizi za kasi ya maisha, familia nyingi hazikai pamoja kama ilivyokuwa zamani. Wengine wanaishi mikoa tofauti, wengine wako nje ya nchi, na wengi humezwa na majukumu ya kazi, masomo na biashara.**

**Hali hii imefanya mawasiliano ya kifamilia kuwa changamoto. Ndipo teknolojia, hususan WhatsApp, ilipojitokeza kama daraja muhimu la kuunganisha familia na kuimarisha undugu.**

**Hata hivyo, faida hii hupatikana pale tu WhatsApp inapotumiwa kwa hekima, adabu na malengo ya kujenga.**

## Undugu huanza na "kuwepo"

Kundi la WhatsApp la familia huwasaidia wanafamilia kujisikia kuwa karibu hata kama wako mbali kijiografia. Ujumbe mfupi wa kusalimiana, kuulizia hali au kutoa taarifa ndogo hujenga hisia ya uwepo na kujali.

Wazee hujiona bado wanahusika katika maisha ya watoto na wajukuu wao, huku vijana wakipata nafasi ya kusikiliza ushauri na hekima ya wakubwa. Kwa njia hii, WhatsApp husaidia kupunguza pengo la kizazi na kuimarisha mshikamano wa kifamilia.

## Kushirikiana taarifa na matukio ya familia

WhatsApp ni jukwaa rahisi la kusambaza taarifa muhimu za kifamilia kwa wakati mmoja. Matukio kama harusi, misiba, kuzaliwa kwa mtoto, kuugua kwa ndugu au mafanikio ya kielimu yanaweza kushirikishwa haraka na kila mwanafamilia akapata taarifa bila usumbufu.

Hili husaidia kila mtu kujisikia kuwa sehemu ya safari ya familia, badala ya kusikia habari hizo baadaye au kupitia watu wa nje.

## Chanzo cha msaada wa kihisia

Moja ya faida kubwa za kundi la familia ni uwezo wake wa kuwa mahali pa faraja na msaada.

Familia inapokumbwa na changamoto, kundi linaweza kuwa nafasi ya kutiana moyo, kuombeana, au kupanga namna ya kusaidia kwa vitendo.

Maneno ya upole, dua na mshikamano unaojengwa kupitia mawasiliano haya huimarisha uhusiano na kuifanya familia iwe nguzo imara wakati wa dhiki.

## Kurahisisha mipango, maamuzi ya kifamilia

Masuala ya kupanga mikutano, sherehe, safari au misaada ya kifamilia huwa rahisi zaidi kupitia WhatsApp.

Badala ya mawasiliano ya pande mbili yanayochosha, kundi huwezesha majadiliano ya pamoja na kufikia maamuzi kwa haraka. Pale panapokuwepo mawasiliano yenye mpangilio na uwazi, WhatsApp hugeuka kuwa chombo cha kuimarisha ushirikiano badala ya chanzo cha mkanganyiko.

## Kubadilishana tamaduni na historia ya familia

Makundi ya WhatsApp huwapa wazee nafasi ya kusimulia historia ya familia, kushirikisha picha za zamani na kueleza mila na desturi za ukoo.

Vijana nao hupata fursa ya kujifunza walikotoka na kujenga fahari ya utambulisho wao. Wakati huohuo, vijana hushirikisha mafanikio na ndoto zao, jambo linalosaidia kuimarisha uhusiano wa pande zote na kujenga heshima ya kizazi kwa kizazi.

## Kueneza ujumbe wa chanya na furaha

WhatsApp ya familia inaweza kuwa chanzo cha furaha na faraja ya kila siku. Ujumbe wa kutia moyo, maneno ya hekima, vichekesho vya heshima na salamu za mapema husaidia kuifanya familia ianze siku kwa tabasamu.

Hata hivyo, chanya hii inahitaji mizani ili isigeuke kuwa kero kwa wengine. Pale ujumbe unapokuwa wa kiasi na wenye maana, huchangia zaidi kuimarisha undugu.

## Umuhimu wa adabu na mipaka

Ili kundi la WhatsApp liwe chombo cha kuimarisha undugu, ni muhimu kuwepo heshima na mipaka. Kauli za dharau, lawama au mabishano makali, hasa kuhusu siasa au masuala nyeti, huweza kuharibu uhusiano.

Kundi la familia linapohifadhiwa kama eneo la heshima, kusikilizana na kutatua tofauti kwa busara, linakuwa mahali salama kwa kila mwanafamilia.

## Kuimarisha ukaribu kupitia sauti na video

Mbali na maandishi, WhatsApp hutoa fursa ya mawasiliano ya sauti na video ambayo huleta ukaribu wa kipekee.

Kusikia sauti ya ndugu au kumuona mzazi kupitia video huamsha hisia za ukaribu ambazo maandishi pekee hayawezi kuzalisha. Mawasiliano haya husaidia kufufua mahusiano na kufanya familia ijisikie kuwa karibu zaidi. Kwa ujumla, ina uwezo wa kuunganisha waliotengana na umbali, kuimarisha mawasiliano na kujenga mshikamano wa kihisia.

Familia itakapokubaliana kutumia WhatsApp kama chombo cha heshima, msaada na mawasiliano chanya, kundi la familia litageuka kuwa kiungo muhimu cha kudumisha upendo na umoja kwa kizazi cha sasa na kijacho.




MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS

# Kwa nini majuto yanatuumiza na namna ya kuyaachia

**Majuto ni miongoni mwa hisia zinazomtesa mtu kimya kimya. Unakuta akili inarudia-rudia tukio la zamani kama filamu: "Laiti nisingesema... laiti nisingechagua... laiti ningethubutu..." Kisaikolojia, majuto ni aina ya maumivu ya ndani yanayotokana na kutazama nyuma na kuhisi kwamba matokeo mabaya yalitokana na maamuzi yetu. Ndiyo maana majuto huambatana na lawama binafsi, aibu, na wakati mwingine hasira ya kujielekezea.**

Kisaikolojia, majuto yanakuja kwa sura mbili: yale ya kufanya kitu kilichoharibu, na yale ya kutofanya kitu ulichopaswa kufanya.

Tafiti nyingi zinaonesha kwamba kwa muda mfupi tunajuta zaidi makosa ya "kitendo," lakini kwa muda mrefu watu hujuta zaidi "fursa walizokosa" au hatua walizoshindwa kuchukua. Hii inaeleza kwa nini majuto ya "laiti ningejitokeza" yanaweza kukaa miaka mingi kuliko majuto ya "nilisema vibaya siku ile."

## Mkosoaji wa ndani au huzuni ya kuombolezwa?

Wanasaikolojia wengi huona majuto kama lugha ya kile kinachoitwa 'inner critic' —sauti ya ndani inayopenda kukuhukumu na kukukatia tamaa. Sauti hii hujaribu kukushawishi kuwa uliteleza kwa sababu "huna uwezo", "huna akili", au "wewe ni mtu wa makosa."

Majuto huweza kutufanya tushindwe kuendelea kwa sababu mkosoaji wa ndani huyaweka makosa kama ushahidi wa udhaifu wetu.

Mtazamo mwingine ni kuyaona kama aina ya maombolezo, yaani kuna kitu tulikipoteza: muda, uhusiano, fursa, heshima, au toleo bora la sisi tunalotamani lingetokea.

Kuyachukulia majuto kama huzuni (grief) hutusaidia kuyashughulikia kwa njia sahihi—kuyakubali, kuomboleza, kisha kuachilia—badala ya kuendelea "kuyarudia" bila kuyamaliza. Hapa ndipo wengi hukwama: tunarudia simulizi la kosa, lakini hatufanyi hatua ya kuponya.

## Kwa nini majuto yanaongezeka zama hizi

Maisha ya sasa yamejaa machaguo nyingi. Kadri machaguo yanavyoongezeka, ndivyo mashaka yanavyoongezeka: "Je, nilichagua sahihi?" Dhana ya 'paradox of choice' inaeleza kuwa wingi wa machaguo unaweza kutufanya tusiridhike na uamuzi tuliochukua, na kuongeza majuto.

Pia, shinikizo la ukamilifu (perfectionism) na hofu ya kuhukumiwa hadharani kwenye mitandao huongeza tabia ya kujilaumu hata kwa makosa madogo.

## Namna ya kuyaachia majuto

Hatua ya kwanza ni kuyatambua majuto kama taarifa, si hukumu ya mwisho juu ya utu wako. Ukiona "nina majuto," jiulize: majuto haya yananionyesha nini ninachokithamini? Labda ni uhusiano, uadilifu, uthubutu, au familia. Ukishajua thamani iliyo nyuma ya maumivu, unaweza kuanza kubadili mwelekeo.

Hatua ya pili ni kuondoa upweke wa majuto. Majuto hustawi kwenye wazo la "ni mimi peke yangu nimefanya upuuzi." Lakini ukweli ni kwamba makosa ni sehemu ya ubinadamu. Kuyakubali kama "kawaida ya maisha" hupunguza aibu na hujenga unyenyekevu. Hili ndilo linalodhoofisha nguvu ya mkosoaji wa ndani.

## Hatua ya tatu ni kuhamisha majuto kutoka jana kwenda kesho.

Badala ya kujiponda, unatazama ukuaji uliotokana na kosa hilo, kisha unaweka ahadi ya vitendo kuhusu mustakabali: "Nitajifunza kuwasiliana mapema," "Nitaweka mipaka," "Nitaomba msamaha," au "Nitajaribu tena." Hapo unabadilika kutoka kuwa mfungwa wa historia kuwa mwanafunzi wa historia.

Hatua ya nne ni mazoezi ya kuandika. Daniel Pink anashauri wazo la 'failure resume'—kuorodhesha "kuanguka" kwako na somo ulilopata, ili ubadilishe aibu kuwa mpango wa kukujenga. Unapoandika, akili hupunguza mzunguko wa mawazo (rumination) na kupata mpangilio.

Hatua ya tano ni kuzungumza na mtu salama. Majuto yakichanganyika na msongo, usingizi kuharibika, au kujihisi huna thamani, msaada wa karibu au wa kitaalamu huwa muhimu. Si kwa sababu wewe ni dhaifu, bali kwa sababu akili inahitaji ushuhuda wa huruma ili ipone.

Mwisho niseme kuwa majuto si adui wa maisha; ni ujumbe unaokuambia kuna thamani muhimu uliyoikosa au uliyoiangusha. Ukijifunza kuyapokea kama huzuni ya kuomboleza, kuyadhoofisha kwa kujionea huruma, na kuyageuza kuwa somo la kesho, majuto huacha kuwa minyororo na hugeuka dira.



# Zijue C saba anazozihitaji kiongozi katika taasisi

**C7 za uongozi imara ni misingi inayojitokeza mara kwa mara katika tafakuri za wasomi wa uongozi. Zimetofautiana kwa majina, lakini kiini chake ni kilekile. Katika makala hii nimekusanya zile C ambazo zimejitokeza mara nyingi na kuunganisha baadhi ili tu tujifunze.**
**Kwa muhtasari, C hizo ni kwanza, confidence (kujiamini), pili, courage (uajsiri), consistency (uthabiti), communication (mawasiliano), compassion (huruma) concentration (kumakinika katika lengo) na creativity (ubinifu).**

### Mawasiliano (communication)

Kwangu, huu ndio msingi muhimu zaidi. Mawasilian ya wazi na ya pande mbili, ni daraja ambalo matokeo yake ni ushirikiano na ufanisi katika taasisi.

Kiongozi anatakiwa asikilize. Kusikiliza huonyesha heshima, huongeza ushirikishwaji, hisia ya umiliki na hivyo kujitoa zaidi. Kiongozi anayesikiliza anaweza kujifunza kitu muhimu, na kuzuia makosa kabla hayajakomaa.

Anapoongea, kiongozi awe muwazi katika malengo, hatua za kufuatwa na sababu ya nini kinafanyika huku akitumia lugha ya kuunganisha, na kuhamasisha watu kufikia lengo.

### Kujiamini (Confidence)

Kiongozi anapojiamini, huwasilisha maamuzi na maono yake kwa uthabiti na kuwajengea wengine imani. Pamoja na uwezekano wa kukosea, hutoa maono, hutetea hoja akiwa imara huku pia akijifunza kutokana na makosa na kuendelea mbele. Bila kujiamini, wazo zuri linaweza kuishia kichwani au kufa kabla ya kutekelezwa.

### Ujasiri (courage)

Uongozi si rahisi. Wakati mwingine unahitaji kufanya jambo gumu—hasa linapokuwa halipendezi kwa baadhi ya watu. Hapa ndipo ujasiri (courage) na msimamo wa ndani (conviction) vinapohitajika.

Ujasiri ni kukabiliana na jukumu linaloonekana gumu na haliwezekani au kupingwa lakini lina maslahi makubwa na mapana. Pia, ni kusema "hapana" inapostahiki.

Kiongozi jasiri hasukumwi na woga wa lawama au kupoteza umaarufu, bali huongozwa na maono na haki. Katika mazingira ya changamoto na mabadiliko, ujasiri huwa ngao inayomsaidia kiongozi kusonga mbele bila kuyumba.

### Huruma (compassion)

Kiongozi anaweza kuwa "mgumu" na bado akawa na huruma. Huruma ni kutambua kuwa watu si idadi ya vichwa; ni maisha yenye mahangaiko, uchovu na mazingira yao. Ukiongoza kazi bila kuongoza mioyo, utaishia kuongoza peke yako. Kiongozi mwenye huruma huunga mkono walio kwenye wakati mgumu, hujali ustawi wao, na husaidia kufunika udhaifu wa timu badala ya kuufichua ili kuwadhalilisha.

### Uthabiti (consistency)

Uthabiti ni muendelezo au kudumu katika msimamo, kusimamia jambo kwa nguvu ileile leo na kesho, lakini pia kuwa na msimamo. Isiwe leo unapanga hivi, kesho unabadilisha, leo unasimamia, kesho unalegea. Hii huua imani na kuharibu nidhamu.

Ndani ya uthabiti kuna kujitoa, yaani kuonesha mfano binafsi kwa kuwekeza muda, nguvu na rasilimali zake ili kufanikisha dira ya pamoja. Mfano, changamoto imetokea, kiongozi anayejitoa hatakaa nyumbani na kupiga simu tu bali ataenda kuongoza timu yake kupambana na dharura husika (ikiwemo ya dharura binafsi ya mfanyakazi) hata kama itambidi akeshe usiku mzima.

### Kumakinika katika malengo, vipaumbele (concentration)

Kujitoa pekee hakutoshi kama huna umakini. Unaweza kuwa na bidii, lakini ukawa unasukuma kila kitu bila mpangilio. Umakini ni uwezo wa kuelekeza nguvu sehemu inayobeba matokeo.

Kiongozi mwenye umakini anajua vipaumbele, anajua nini kifanyike sasa na nini kitasubiri, na anajua nini kikabidhiwe kwa wengine. Umakini humsaidia kiongozi kudhibiti msukumo wa "kufurahisha kila mtu" na kufanya kila kitu kwa ufanisi mdogo.

### Ubunifu (creativity)

Ubunifu ni uwezo wa kuona njia mpya pale njia ya jana haifanyi kazi. Changamoto zinapokuja, kiongozi mbunifu huuliza: "Tunaweza kufanya nini tofauti?" Huona fursa ndani ya kikwazo, na hujenga mazingira ambayo watu hawatishwi na mawazo mapya.

Ubunifu huipa taasisi uwezo wa kubaki imara hata mazingira yakibadilika.

### C ya nyongeza: Udadisi wa kujifunza (curiosity)

Hii ni nyongeza muhimu sana. Kiongozi bora habaki kwenye nafasi ya "mimi ni mtaalamu, najua kila kitu." Anakaa kwenye nafasi ya mwanafunzi. Badala ya kukimbilia hitimisho, huuliza maswali sahihi, huchunguza taarifa, na hutafuta kuelewa kabla ya kuhukumu. Udadisi huu huongeza hekima, huondoa majibu ya pupa, na huifanya timu ijisikie salama kutoa mawazo kwa sababu kiongozi hasimami kwenye dhana, bali kwenye uelewa.